Ziada
FUND

# WARAKA WA OFA

**Tarehe ya Ufunguzi wa Mauzo ya Awali: 26 Januari 2026**
**Tarehe ya Kufungwa kwa Mauzo ya Awali: 25 Februari 2026**
**Tarehe ya Kuanza kwa Sera ya Bima: 26 Januari 2026**
**Tarehe ya Kutangazwa kwa Matokeo: 09 Machi 2026**
**Bei ya Kipande Kimoja Kwenye Mauzo ya Awali: TZS100**

APeF
Asset Management and Pension

2026
Unastahili Zaidi

**AFRICA PENSION FUND LIMITED**

# MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA WA ZIADA WENYE MANUFAA YA BIMA YA MAISHA

## MFUKO WA ZIADA

## WARAKA WA TOLEO

Mfuko wa Uwekezaji wa Ukuaji Usio na Kikomo

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya Ufunguzi wa Mauzo ya Awali:** | **26 Januari 2026** |
| **Tarehe ya Kufungwa kwa Mauzo ya Awali:** | **25 Februari 2026** |
| **Tarehe ya Kuanza kwa Hati ya Bima:** | **26 Januari 2026** |
| **Tarehe ya Kutangazwa kwa Matokeo:** | **09 Machi 2026** |
| **Bei ya kipande:** | **TZS 100/=** |

Waraka huu unaeleza kwa ufupi, habari kuhusu Mfuko wa Ziada. Mwekezaji mtarajiwa anapaswa kusoma waraka huu kabla ya kuwekeza. Waraka huu utunzwe kwa marejeo ya baadae.

Waraka huu utaendelea kutumika hadi hapo mabadiliko yatakapotokea na mabadiliko hayo yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa ajili ya kupitishwa kabla ya kusambazwa kwa wenye vipande.

**TAHADHARI / ONYO**

Maelezo ya Mfuko yameandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 kama ilivyorekebishwa na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifumo ya Uwekezaji wa Pamoja) za mwaka 1997, Sheria za Makampuni na 212 (sheria na 12 ya 2002), Gazeti la Serikali Na.770 la mwaka 1997.

Waraka huu umeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana (CMSA). Vipande vinavyouzwa na Mfuko huu havijaidhinishwa au kutoidhinishwa na Mamlaka hayo.

Wawekezaji watarajiwa, wanapaswa kuwa waangalifu katika kutafakari mambo yaliyoelezwa chini ya Ibara ya "Hatari za Uwekezaji" (Risk Factors). Ikiwa una mashaka yoyote kuhusiana na yaliyomo katika waraka huu, unapaswa kushauriana na Dalali wako wa Soko la Hisa, Meneja wa Benki, Mwanasheria, Mhasibu au Mshauri Mwingine wa Mambo ya Uwekezaji.

**THAMANI HALISI YA KIPANDE PAMOJA NA MAPATO YAKE YANAWEZA KUPANDA AU KUSHUKA.**

## 1. MAMBO MUHIMU KUHUSU MFUKO WA ZIADA

**Madhumuni ya Mfuko:** Mfuko wa Ziada ni mfuko ulio wazi unaokusudia kukuza mtaji kwa muda mrefu, huku pia ukitoa fao la bima ikiwemo Bima ya Maisha, Ulemavu wa Kudumu na Gharama za Mazishi.

- **Nani Anaweza Kuwekeza**: Mfuko upo wazi kwa ajili ya uwekezaji kwa watu wote walio ndani na nje ya nchi, ikiwemo mifuko ya pensheni, mabenki, mashirika ya serikali, Mamlaka za Udhibiti, Asasi za kiraia (NGOs), na mashirika mengine ya kibiashara.
- **Ukwasi**: Uuzaji wa vipande utafanyika kila siku ya kazi baada ya kumalizika kipindi cha mauzo ya awali. Mwekezaji atapokea malipo ya mauzo ya vipande ndani ya siku tatu za kazi baada ya kutuma maombi ya mauzo. Fedha za mauzo zitatumwa moja kwa moja katika akaunti ya benki ya mwekezaji au simu ya mkononi iliyosajiliwa.
- **Thamani ya Awali ya Kipande**: Thamani ya awali ya kipande kimoja ni Shilingi 100.
- **Bei ya Kipande**: Vipande vitauzwa kwa bei ya Shilingi 100 kwa kila kipande wakati wa kipindi cha mauzo ya awali (yaani kuanzia tarehe 26 Januari 2026 hadi 25 Februari 2026), na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani ya halisi ya kipande ya wakati huo (Net Asset Value).
- **Kima cha Chini cha Kuwekeza:** Kima cha chini cha kuwekeza ni shilingi 50,000/= na baada ya hapo unaweza kuwekeza shilingi 10,000/= na kuendelea.
- **Kwango cha Juu cha Kuwekeza:** Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza, mwekezaji anaweza kuwekeza kiwango chochote.
- **Umiliki:** Umiliki unaweza kuwa kwa mtu mmoja (single) au watu wawili (jointly).
- **Uwazi:** Mfuko huu utatangaza thamani ya kipande ndani ya siku 10 za kazi baada ya tarehe ya awali ya kufungwa kwa mauzo na baada ya hapo bei hiyo itatangazwa kila siku ya kazi.
- **Sera ya Uwekezaji:** Mfuko utawekeza fedha zake zote katika masoko ya fedha yanayotoa mapato ya kudumu kama vile dhamana za serikali. Hakuna uwekezaji katika hisa utafanywa na mfuko huu.
- **Ada ya kungia na kutoka:** Hakutakuwa na ada ya kuingia wala ada ya kutoka kwenye mfuko.
- **Hatari za Uwekezaji:** Wawekezaji watarajiwa, wanapaswa kuwa waangalifu katika kutafakari mambo yaliyoelezwa chini ya Ibara ya "Hatari za Uwekezaji" (Risk Factors).
- **Faida za Bima ya Maisha (Kifo au Ulemavu wa Kudumu):** Faida ya bima ya maisha itatoa bima sawa na asilimia 50 ya Thamani Halisi ya Mali (NAV) iliyopo, kwa sharti kwamba NAV ya chini inayostahili ni TZS 250,000 na kiwango cha juu cha bima ni TZS 100,000,000. Faida hii itatumika tu endapo NAV haijashuka chini ya TZS 250,000 katika kipindi chochote cha miezi sita (6) iliyotangulia.
- **Mipaka ya Fao la Bima:** Bima inapatikana kwa wawekezaji wenye umri wa miaka 18 mpaka miaka 60.
- **Gharama za Mazishi kwa mtoto:** Kiwango cha juu cha fao la mazishi ni shilingi 1,000,000 kutegemea na thamani halisi ya kipande (Net Asset Value).

**TAARIFA YA WAJIBU WA WAKURUGENZI WA MENEJA**

Waraka huu wa Toleo umepitishwa na kuidhinishwa na Wakurugenzi wa Africa Pension Fund Limited. Kwa pamoja na kila mmoja binafsi wanakubali kuwajibika kikamilifu kwa usahihi wa taarifa zote zilizomo humu na wanathibitisha kwamba, baada ya kufanya uchunguzi wote unaofaa kwa mazingira yaliyopo, kwa uelewa na imani yao, hakuna taarifa yoyote muhimu iliyotolewa ambayo ingeweza kufanya taarifa yoyote ndani ya waraka huu kuwa ya kupotosha.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imeidhinisha Mauzo haya ya vipande vya mfuko wa Ziada (Ziada Fund Unit Trust Scheme), na idhini hiyo haipaswi kutafsiriwa kuwa Mamlaka inapendekeza uwekezaji huu.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana haitawajibika kwa upungufu wowote wa taarifa uliofanywa na Africa Pension Fund Limited na haihusiki na yaliyomo katika Waraka huu, na haitoi uwakilishi wowote kuhusu usahihi au ukamilifu wake na inakanusha waziwazi uwajibikaji wowote kwa hasara yoyote itakayotokea kwa namna yoyote kutokana uwekezaji katika mfuko huu.

Waraka huu utaendelea kutumika hadi hapo mabadiliko yatakapotokea na mabadiliko hayo yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa ajili ya kupitishwa kabla ya kusambazwa kwa wenye vipande.

**MFUKO WA ZIADA**

**(Umeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)**

**MENEJA WA MFUKO**
Africa Pension Fund Limited (APeF)
153, Barabara ya Haile Selassie
Ghorofa ya Pili
S.L.P. 6422
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.apef.co.tz

**WAKALA WA BIMA**
Alliance Life Assurance Limited
Jengo la Exim Tower, Ghorofa ya Tano, Mtaa wa Ghana
S.L.P. 11522
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.alliancelife.co.tz

**MDHAMINI WA MFUKO**
National Bank of Commerce Limited
Makao Makuu, Sokoine Drive & Azikiwe Street
S.L.P. 1863
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.nbc.co.tz

**MSAJILI WA MFUKO**
Africa Pension Fund Limited
S.L.P. 6422
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.apef.co.tz

**WAKAGUZI WA MAHESABU**
RSM East Africa
1040, Barabara Ya Haile Selassie,
S.L.P. 79586
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.rms.global/tanzania

**WANASHERIA**
IMMMA Advocates
357, Barabar ya United Nations
S.L.P. 72484
Dar es Salaam, Tanzania
Tovuti: www.immma.co.tz

Wadhamini wa mfuko wa Ziada, ambao majina yao yameorodheshwa hapa chini wanakubali kuwajibika kwa taarifa zilizomo katika waraka huu, kwamba ni sahihi hadi kufikia tarehe ya kuchapishwa kwa waraka huu.

**MAJINA YA WADHAMINI:**

National Bank of Commerce Limited – Mdhamini wa mfuko

**Tarehe:** **2026**

## MAANA YA MANENO / TAFSIRI

**"Tarehe ya Kukubaliwa" au "Tarehe ya Kukubali"** inamaanisha tarehe ambayo malipo na fomu za maombi au taarifa ya akaunti na maombi ya mauzo ya vipande yatapokelewa. Maombi hayo yatapokelewa ndani ya saa za kazi (yaani kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri) na Meneja wa mfuko au wakala aliyeidhinishwa na Meneja wa mfuko.

**"Sheria"** inamaanisha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Cap 79 ya mwaka 1994 (kama ilivyofanyiwa marekebisho) na kanuni zilizotungwa chini yake.

**"Mamlaka"** inamaanisha Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana iliyoanzishwa chini ya Sheria hiyo.

**"Africa Pension Fund"** inamaanisha kampuni iliyosajiliwa chini ya Bodi ya Wakurugenzi wa Africa Pension Fund Limited (APeF).

**"Tarehe za Kufunga Vitabu"** Inamaanisha tarehe ambazo rejesta ya wamiliki wa vipande hufungwa kwa madhumuni ya usimamizi wa mgawanyo wa vipande au sababu nyingine yoyote.

**"Raia"** inamaanisha raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya mwaka 1995.

**"Tarehe ya Mauzo ya Awali"** inamaanisha tarehe ambayo Meneja wa mfuko anauza vipande kwa umma mara ya kwanza chini ya mfuko huu (yaani 26 Januari 2026).

**"Kamishna wa Bima"** inamaanisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Bima.

**"Mdhamini wa Mfuko"** ni taasisi inayohusika na kusimamia fedha za mfuko kwa niaba ya wamiliki wa vipande kwa mujibu wa makubaliano ya Waraka wa Makubaliano.

**"Waraka wa Makubaliano" (Deed of Trust)** inamaanisha hati ya dhamana inayojumuisha Mfuko wa Ziada uliounganishwa na bima uliosainiwa siku ya tarehe 29 Julai 2025.

**"Mauzo ya Awali"** ni uuzaji wa vipande vya Mfuko huu kuanzia tarehe ya kuanza hadi kipindi maalum kilichoamuliwa na meneja wa Mfuko.

**"Sheria ya Bima"** inamaanisha Sheria ya Bima ya mwaka 2009 na kanuni zilizotungwa chini yake.

**"Hati ya Bima"** inamaanisha bima ya maisha, ulemavu wa kudumu na gharama za mazishi kama ilivyoanishwa na Meneja wa Mfuko na mtoa bima, na kuambatanishwa kwenye waraka wa makubaliano.

**"Malipo ya Bima"** inamaanisha kiasi cha fedha kinacholipwa kwa mtoa bima kila mwaka kutoka kwenye Mfuko huu, ili kumpatia mwanachama Fao la Bima.

**"Mtoa Bima"** ni kampuni yoyote ya bima inayotoa bima ya maisha na/au isiyo ya maisha ikiwa ni pamoja na bima ya ajali binafsi, gharama za mazishi, n.k.

**"Kipindi cha utulivu wa Mfuko"** ni kipindi kisichozidi siku 10 za kazi kinachoanza mara baada ya kufungwa kwa mauzo ya awali na wakati ambao shughuli za ununuzi na uuzaji wa vipande hautofanyika chini ya Mfuko huu.

**"Mwekezaji"** ni mtu ambaye amenunua vipande chini ya Mfuko huu.

**"Mfuko"** ni Mfuko wa Ziada wa uwekezaji wa masoko ya fedha ulioambatanishwa na bima kama ilivyoainishwa kwenye waraka wa makubaliano.

**"Thamani halisi ya kipande"** ni thamani inayopatikana kwa kutoa madeni ya Mfuko huu kutoka kwenye jumla ya mali zake.

**"Waraka wa Toleo"** ni nyaraka hii ya tarehe ya 26 Januari 2026.

**"Ununuzi wa vipande"** inamaanisha mwekezaji anauza vipande vyake kiasi au vyote na kurudishwa kwa Meneja wa Mfuko.

**"Rejesta"** ni daftari la wamiliki wa vipande.

**"Uuzaji"** inamaanisha mauzo ya awali na mauzo yajayo.

**''Mauzo ya Awali**: Kuanza kuuza vipande wakati wa kipindi cha mauzo ya awali

**'Mauzo ya baadae**: Kuanza kuuza vipande baada ya kufungwa kwa mauzo ya awali

**"Taarifa ya Akaunti"** ni taarifa ya kifedha inayotolewa na Mfuko kwa mwekezaji wa kipande ikionyesha idadi ya vipande anavyomiliki.

**"Kipande"** ni sehemu ya umiliki wa mali za Mfuko.

**"Mwekezaji wa Vipande"** ni mtu anayekubalika kisheria na Mfuko kama mwekezaji halali wa vipande.

**"Siku ya Kazi"** ni siku yoyote isipokuwa Jumamosi, Jumapili au siku ambayo soko kuu la hisa litakuwa limefungwa.

**KAULI YA MWENYEKITI**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Africa Pension Fund Limited

Kwa heshima kubwa ninawasilisha Waraka huu wa Utoaji wa Ofa kwa ajili ya Mfuko wa Ziada, kama kielelezo cha dhamira ya dhati ya Africa Pension Fund katika kutoa suluhisho zenye maana, zenye mtazamo wa mbele, na zenye ubora wa hali ya juu. Bodi imepitia kwa makini na kuidhinisha waraka huu na inaridhika kikamilifu kwamba unaonyesha kwa usahihi, uhalisia na usawa muundo, malengo na hatari zilizomo ndani ya Mfuko. Uundaji wa Mfuko wa Ziada umeongozwa na mfumo thabiti wa utawala bora na kutekelezwa kwa umakini wa hali ya juu, kwa kuzingatia Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja), Tangazo la Serikali Na. 770 la mwaka 1997. Kila jitihada zimefanyika kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu zimewekwa wazi na taarifa zilizomo humu ni sahihi na kamili kwa kiwango cha juu cha uelewa na imani yetu kama ya tarehe ya kuidhinishwa.

**KAULI YA MKURUGENZI MTENDAJI**

Ninapenda kuthibitisha dhamira yetu ya kudumisha viwango vya juu vya uwazi, uwajibikaji na utii wa kanuni katika kuandaa na kutoa Mfuko wa Ziada. Katika kuandaa waraka huu, uongozi wa APeF umetumia umakini na uangalifu kuhakikisha kuwa taarifa zilizotolewa ni kamili, sahihi na zinazingatia kikamilifu mfumo wa udhibiti unaowekwa na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja), Tangazo la Serikali Na. 770 la mwaka 1997.

Tumekuwa makini katika kuhakikisha tunazingatia kanuni za uadilifu, uwazi na ulinzi wa wawekezaji katika hatua zote za maendeleo ya bidhaa na utoaji wa taarifa. Lengo letu kupitia Mfuko wa Ziada ni kutoa suluhisho la uwekezaji lenye uhakika na linalobadilika kulingana na mahitaji, likiwa na mchango katika ujumuishaji wa kifedha na likikidhi mahitaji ya wawekezaji wa taasisi na binafsi. Tunaendelea kujitolea kudumisha utawala bora, nidhamu katika usimamizi wa fedha na utamaduni thabiti wa utii wa kanuni unaoweka maslahi ya wawekezaji wetu mbele. Tunawaalika mpitie ofa hii kwa kujiamini, mkijua kuwa inaakisi sio tu fursa madhubuti ya uwekezaji, bali pia viwango vya juu tunavyojipima navyo kama wasimamizi wa mtaji wenu.

**TAARIFA YA MTIZAMO WA MBELENI**

*Africa Pension Fund Limited*

Waraka huu wa Ofa unajumuisha taarifa zenye mtazamo wa mbele zinazoakisi mwelekeo wa kimkakati na matarajio ya Africa Pension Fund katika nafasi yake kama Msimamizi wa Mfuko wa Ziada.

Tunaamini kuwa Mfuko wa Ziada umeandaliwa kwa upekee ili kutoa mapato ya uhakika na salama kupitia uwekezaji katika vyombo kama hati fungani za serikali za muda mfupi (Treasury bills), hati fungani za muda mrefu (Treasury bonds) na madeni ya kampuni zenye ubora wa juu. Lengo letu ni kuwapatia wawekezaji suluhisho salama, lenye hatari ndogo, linalopatikana kwa urahisi na lenye mchango katika mipango ya kifedha pamoja na faida ya kinga ya bima yenye maana.

Tunatarajia ongezeko la hamasa kutoka kwa watu binafsi na taasisi nchini Tanzania na kanda nzima kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya suluhisho za kifedha zenye kinga ya bima. Tunapoendelea mbele, tutaendelea kuwekeza katika ubunifu, upatikanaji wa kidijitali na uwazi ili kuboresha uzoefu wa wawekezaji.

Ingawa tuna imani na mwelekeo wa Mfuko, tunatambua kuwa mienendo ya soko hubadilika. Mambo ya kiuchumi, mabadiliko ya viwango vya riba na hali za nje yanaweza kuathiri utendaji. Pamoja na hayo, APeF inabaki imara katika kujitolea kwa usimamizi makini, utiifu wa kanuni na ustawi wa kifedha wa muda mrefu wa wawekezaji wetu.
Tunawashukuru kwa kuendelea kuiamini Africa Pension Fund.

**TAMKO LA BODI**

Waraka huu wa Ofa umepitiwa na kuidhinishwa na Wakurugenzi wa Africa Pension Fund Limited ambao kwa pamoja na binafsi wanakubali kuwajibika kikamilifu kwa usahihi wa taarifa zote zilizomo humu na wanathibitisha kuwa, baada ya kufanya uchunguzi unaostahili katika mazingira haya, kwa kiwango cha juu cha uelewa na imani yao, hakuna taarifa nyingine iliyokosekana ambayo inaweza kufanya taarifa yoyote humu kuwa ya kupotosha.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imeidhinisha utoaji, ofa au mwaliko unaohusu Mfuko wa Ziada, ambao ni Mfuko wa Uaminifu wa Uwekezaji Uliounganishwa na Bima, ambao ni mada ya waraka huu wa ofa. Uidhinishaji huu hautafsiriwi kuwa Mamlaka inapendekeza uwekezaji huu.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana haitawajibika kwa upungufu wowote wa taarifa kutoka kwa Africa Pension Fund Limited, na haina wajibu wa maudhui ya waraka huu wa ofa, wala haihakikishi usahihi au ukamilifu wake, na inajiondoa wazi kwa dhima yoyote itakayotokea kutokana na utegemezi wa taarifa zote au sehemu ya maudhui ya waraka huu.

Waraka huu wa Ofa utaendelea kuwa sahihi hadi pale mabadiliko makubwa yatakapotokea (yasiyohusiana na mabadiliko ya sifa za msingi na ndani ya wigo wa waraka huu), na baada ya hapo mabadiliko hayo yatapelekwa kwa Mamlaka kwa idhini na kusambazwa kwa wamiliki wa vipande vya mfuko.

_______________ ___________________ ____________________

**Mkurugenzi Katibu**

## YALIYOMO

TAHADHARI / ONYO ..... ii
MAMBO MUHIMU KUHUSU MFUKO WA ZIADA ..... iii
TAARIFA YA WAJIBU WA WAKURUGENZI WA MENEJA ..... iv
MFUKO WA ZIADA ..... v
MAANA YA MANENO / TAFSIRI ..... vi
KAULI YA MWENYEKITI ..... vii
KAULI YA MKURUGENZI MTENDAJI ..... vii
TAARIFA YA MTIZAMO WA MBELENI ..... viii
TAMKO LA BODI ..... viii
1. HISTORIA ..... 4
2. UTANGULIZI ..... 4
3. MENEJA/MSIMAMIZI WA MFUKO ..... 4
4. BODI YA WAKURUGENZI ..... 4
5. KAMATI YA UWEKEZAJI ..... 8
6. MENEJIMENT YA MFUKO ..... 8
7. MAJUKUMU YA MENEJA WA MFUKO ..... 10
8. MTOA BIMA WA MFUKO WA ZIADA ..... 11
9. MDHAMINI WA MFUKO WA ZIADA ..... 11
10. WATU WANAOHUSIANA ..... 12
11. RATIBA YA TOLEO ..... 12
12. TAMKO LA UZINGATIAJI WA SHERIA KUTOKA KWA MENEJA WA MFUKO ..... 13
13. GHARAMA ZA AWALI ZA UUZAJI WA VIPANDE ..... 13
14. HATARI ZA UWEKEZAJI ..... 13
15. TAARIFA ZA MFUKO ..... 14
16. MALENGO YA MFUKO ..... 14
17. WAWEKEZAJI WANAOSTAHILI KUWEKEZA ..... 14
18. KIASI CHA UWEKEZAJI ..... 14
19. BEI YA KIPANDE ..... 14
20. ADA YA KUINGIA ..... 15
21. UKWASI/ KUUZA VIPANDE ..... 15
22. FAIDA (FAO) ZA BIMA KATIKA MFUKO WA ZIADA ..... 15
23. MASHARTI NA VIGEZO VYA BIMA ..... 16

24. FAIDA YA GHARAMA ZA MAZISHI .......... 16

25. UTARATIBU WA FAO LA BIMA .......... 17

26. FAO LA BIMA - WAKATI WA KIFO .......... 17

27. FAO - KWA ULEMAVU KAMILI NA WA KUDUMU .......... 17

28. WAJIBU WA MENEJA KUSHUGHULIKIA MADAI YA BIMA .......... 17

29. MASHARTI YA KUINGIA KWENYE MFUKO .......... 17

30. MALIPO YA KIWANGO CHA BIMA .......... 17

31. RATIBA YA MALIPO YA KIWANGO CHA BIMA .......... 19

32. KIFUNGU CHA MAPITIO CHA HATI YA BIMA YA KIKUNDI .......... 19

33. UUZAJI WA VIPANDE .......... 19

34. TAARIFA YA AKAUNTI .......... 19

35. UWEKEZAJI NA ZUIO LA MIKOPO .......... 20

36. SERA YA UWEKEZAJI .......... 20

37. UTHAMINI WA MALI ZA MFUKO .......... 20

38. UTEUZI WA MRITHI (NOMINEE) .......... 20

39. NJIA ZA UMILIKI WA VIPANDE .......... 21

40. MUUNDO WA HATI YA BIMA .......... 21

41. MASHARTI MENGINE YA BIMA .......... 21

42. DHAMANA YA MKOPO AU KUHAMISHA FAO LA BIMA. .......... 21

43. UWEZO WA KUHAMIA MIFUKO MINGINE .......... 21

44. MAOMBI ZAIDI YA MOJA KUTOKA KWA MWEKEZAJI MMOJA .......... 21

45. UNUNUZI WA VIPANDE .......... 22

46. MALIPO YA UNUNUZI WA VIPANDE .......... 22

47. MANUNUZI YA VIPANDE BAADA YA KIPINDI CHA AWALI .......... 22

48. MIAMALA YA WASHIRIKA .......... 23

49. MAONI NA MALALAMIKO YA MWEKEZAJI .......... 23

50. GHARAMA ZA MFUKO .......... 23

51. UTHAMINI WA THAMANI HALISI YA VIPANDE .......... 24

52. HAKI NA HUDUMA KWA WAWEKEZAJI WA VIPANDE .......... 25

53. UHUSIANO KATI YA BEI YA MANUNUZI AU MAUZO NA THAMANI HALISI YA KIPANDE (NET ASSET VALUE - NAV) .......... 25

54. MAZINGIRA YANAYOWEZA KUFANYA SHUGHULI ZA MFUKO KUAHIRISHWA AU KUFUNGWA .......... 25

55. KIPINDI KATI YA KUPOKEA OMBI LA UUZWAJI VIPANDE NA MALIPO YA FEDHA .......... 26

56. KODI ..... 26

57. UKOMO WA MFUKO ..... 26

58. MAELEZO YA UJUMLA ..... 26

59. ADA NA MAKATO ..... 27

60. KIFO CHA MWEKEZAJI ..... 27

61. MANUFAA YATAKAYOTOLEWA WAKATI WA KIFO ..... 27

62. MANUFAA YATAKAYOTOLEWA – ULEMAVU WA WAKUDUMU ..... 28

63. MIKUTANO ..... 28

## 1. HISTORIA

Africa Pension Fund Limited (APeF) ni meneja wa mifuko ya uwekezaji aliyepewa leseni na kusimamiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya Tanzania. Kampuni hii inatoa huduma za kitaalamu za usimamizi wa uwekezaji na ushauri wa kifedha zenye lengo la kuwasaidia wawekezaji kujenga usalama wa kifedha wa muda mrefu. APeF inasimamia mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uwekezaji wa taasisi unaolenga kutoa mapato tulivu, kuhifadhi mtaji na kuhakikisha uwazi katika utoaji wa taarifa. Kampuni inashirikiana na taasisi kuu za kifedha kuhakikisha utawala bora, ufanisi wa uendeshaji na ulinzi wa wawekezaji. Kupitia taratibu za uwekezaji zenye nidhamu na ufuatiliaji endelevu wa soko, APeF inalenga kuwapa wawekezaji uhakika kwamba akiba zao zinasimamiwa kwa uwajibikaji na kwa mujibu wa malengo yao ya kifedha.

## 2. UTANGULIZI

Mfuko wa Ziada ni Mfuko wa uwekezaji wa pamoja kwenye masoko ya fedha na mitaji, ulioambatanishwa na faida za bima ikiwa ni pamoja na b**ima ya maisha, ulemavu wa kudumu**, na g**harama za mazishi**. Mfuko huu utatoa faida zifuatozo:

- Bima ya Maisha
- Uwekezaji na akiba
- Urahisi wa kuingia na kutoka kwenye Mfuko

## 3. MENEJA/MSIMAMIZI WA MFUKO

Mfuko huu wa Ziada unasimamiwa na Africa Pension Fund Limited (APeF) pamoja na Bodi ya Wakurugenzi. Bodi hii ya wakurugenzi imeweka muundo wa usimamizi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kila siku za mfuko.

## 4. BODI YA WAKURUGENZI

**Bw. Yogesh Manek – Mwenyekiti wa Bodi**

Bw. Yogesh Manek ni mwanzilishi mkuu na Mwenyekiti Mtendaji wa Mac Group Ltd, taasisi kubwa ya biashara nchini Tanzania yenye uwekezaji mpana katika sekta mbalimbali ikiwemo utengenezaji wa bidhaa, benki, bima, mali isiyohamishika, kilimo-biashara, madini, na usafirishaji. Katika kipindi cha takriban miaka 40, amechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa taasisi hii, akiivusha katika mazingira ya ki-uchumi yenye changamoto pamoja na yale ya soko huria. Mtandao wake mpana wa washirika wa kibiashara barani Afrika, Asia, Ulaya na Amerika unaonesha ushawishi wake wa kimkakati katika kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mbali na ujuzi wake wa kibiashara, Bw. Manek anachangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha mfumo wa uchumi wa Tanzania. Yeye ni miongoni mwa waanzilishi wa Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) na Jukwaa la Wakurugenzi Wakuu (CEO's Forum), taasisi ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza sera rafiki kwa biashara na mageuzi ya sekta mbalimbali. Ameshiriki katika bodi nyingi za ushauri serikalini, akichangia kuandaa sera zinazoiweka Tanzania kuwa pendekezo la kwanza kwa wawekezaji wa kimataifa.

Bw. Manek ni mjumbe wa bodi za makampuni zaidi ya 25 maarufu, zikiwemo Kampuni ya bima ya Heritage, Strategis na Alliance Life Assurance, pamoja na kampuni ya Africa Pension Fund (APeF)na pia alikuwa mjumbe wa Bodi ya Benki ya NBC Tanzania. Nje ya shughuli za kibiashara, amejitolea kwa huduma za kijamii na maendeleo ya jamii akiwa Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shree Goverdhannathji Haveli na Mwenyekiti wa Dar Business Group, jambo linaloonesha dhamira yake kwa ustawi wa jamii.

**Bw. Shaffin Jamal – Mkurugenzi wa Bodi**

Bw. Shaffin J.H. Jamal ni mjasiriamali mahiri na kiongozi mwenye uzoefu mpana katika sekta mbalimbali nchini Tanzania. Tangu mwaka 1997, amekuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Union Trust Investments Ltd., ambapo anasimamia biashara zenye wigo mpana, ikiwemo huduma za fedha, malazi, chakula na kilimo. Pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Union Trust Hospitality Group, inayosimamia hoteli za hadhi ya juu jijini Arusha, pamoja na Union Trust Properties Ltd., ambayo imebobea katika uendelezaji wa majengo ya kibiashara, makazi, na viwanda.

Katika sekta ya kifedha, Bw. Jamal ameshika nyadhifa muhimu ikiwa ni pamoja na kuwa Mwenyekiti wa kampuni ya bima ya Alliance Insurance Corporation na Alliance Life Assurance Company, na pia alikuwa ni Mkurugenzi wa benki ya NBC Tanzania. Uongozi wake unavuka mipaka ya kitaifa akiwa pia ni Mwenyekiti wa kampuni ya bima ya Alliance Africa General Insurance nchini Uganda.

Mbali na mafanikio ya kibiashara, Bw. Jamal anajihusisha kikamilifu na mashirika ya kijamii na kitaaluma, ikiwa ni pamoja na Baraza la Kitaifa la Aga Khan, CEO Roundtable ya Tanzania, na pia kama Mwenyekiti Mwanzilishi wa Young Presidents Organization (YPO) nchini Tanzania.

Bw. Jamal ana shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (MBA) iliobobea Usimamizi wa Kimataifa kutoka chuo kikuu cha American International kilichopo Uingereza. Aidha, amehitimu programu za uongozi katika chuo kikuu cha biashara cha Harvard na Chuo Kikuu cha Stanford, jambo linaloonesha ujuzi wake katika uongozi na Uchumi. Elimu yake ya kimataifa na mtandao wake wa kitaaluma vinaonyesha uwezo wake wa kuongoza ukuaji wa kimkakati na kuendeleza ushirikiano wenye tija.

**Bw. Sadi Shemliwa – Mkurugenzi wa Bodi**

Bw Sadi Waziri Shemliwa ni mshauri katika Sayansi ya Hesabu za Bima (Actuarial Science), Usimamizi wa Hatari za Kibiashara (Enterprise Risk Management), na Ulinzi wa Kijamii (Social Protection), akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 25. Yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Actuarial and Risk Consulting (T) Limited, Raisi wa Chama cha Wanahesabu wa Bima Tanzania (Actuarial Society of Tanzania), na Mkurugenzi wa Actuarial Risk and Consulting (T) Limited pamoja na Africa Pension Fund Limited. Utaalamu wake unahusisha tathmini za kihesabu za bima, mifumo ya usimamizi wa hatari, na mipango ya kimkakati kwa taasisi za serikali na binafsi. Amefanya kazi na Wizara ya Afya, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, na mashirika ya kimataifa kama Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika miradi mbalimbali.

Akiwa ni mhadhiri na mkufunzi, Bw.Sadi amewahi kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Usimamizi wa Fedha (IFM), akifundisha masuala ya hesabu za bima na usimamizi wa hatari. Ana shahada za juu zikiwemo MSc katika Usimamizi wa Hesabu za Bima (Actuarial Management) na MSc katika Sayansi ya Hesabu za Bima kutoka chuo kikuu cha City mjini Uingereza. Pia amepata vyeti vya kitaalamu kama vile Certified Enterprise Risk Manager na ISO 9001 Quality Management Lead Auditor (Msimazi vihatarishi katika Biashara Aliyethibitishwa). Uwezo wake maalum unahusisha kubuni na kupangilia bei ya bidhaa za bima, kufanya tathmini za pensheni za kihesabu, na utungaji wa sera, jambo linaloonyesha umahiri wake katika huduma za kihesabu na usimamizi wa hatari.

Mafanikio mengine katika kazi ya Bw. Sadi ni pamoja na kuongoza utekelezaji wa mfumo wa Usimamizi wa Hatari za Kibiashara na Mipango ya Uendelevu wa Biashara (Business Continuity Programs) katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) hapa Tanzania, pamoja na kusaidia taasisi hiyo kupata cheti cha ISO 9001:2008.

**Bi. Geetha Sivakumar – Mkurugenzi wa Bodi**
Geetha Sivakumar ni mwekezaji mwenye uzoefu na mkurugenzi wa kampuni ambaye amejenga taaluma ya zaidi ya miaka 24 katika kusimamia na kuongoza shughuli mbalimbali katika sekta mbalimbali kama vile bima, benki, viwanda, usafirishaji na ugavi, kilimo, madini, na mali isiyohamishika. Tangu mwaka 2004, amekuwa Mkurugenzi katika MAC Group Ltd, akiongoza mwelekeo wa kimkakati wa kampuni na kuhakikisha mikakati hiyo inaendana na malengo ya muda mrefu ya kikundi.

Geetha pia ni mkurugenzi katika kampuni tanzu kadhaa za MAC Group, zikiwemo Strategis Insurance Tanzania Ltd, Grand Reinsurance Tanzania Ltd, na Africa Pension Fund Ltd, miongoni mwa zingine. Utaalamu wake unajumuisha upangaji wa mikakati, uchambuzi wa kifedha, utawala wa mashirika, na mikakati ya uwekezaji. Ameongoza utekelezaji wa mikakati ya uwekezaji inayolenga kukuza ukuaji endelevu huku ikihakikisha mapato ya juu, pamoja na kuongoza kamati za ukaguzi na hatari na kusimamia mifumo madhubuti ya utawala kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji.

Uongozi wake unajulikana kwa ushirikiano mzuri na wadau na mafanikio katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo huimarisha ukuaji na ustahimilivu wa mashirika. Kwa upande wa elimu, Geetha ana Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) kutoka Edinburgh Business School ya Chuo Kikuu cha Heriot-Watt, na Shahada ya Uzamili ya Biashara (M.Com) kutoka Chuo Kikuu cha Madras, India. Uzoefu wake katika Uhasibu wa Kitaaluma (Chartered Accountancy) unazidi kuimarisha umahiri wake katika uchambuzi wa fedha na masuala ya uzingatiaji wa sheria, na kumfanya kuwa mmoja wa watu muhimu katika mafanikio ya MAC Group.

**Dkt. Hamisi S. Kibola – Mkurugenzi wa Bodi**
Dkt. Hamisi S. Kibola ni mwanasheria na mtaalamu wa masuala ya fedha mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka arobaini katika sekta za sheria, fedha, na udhibiti. Ana shahada ya Sheria (LLB Hons), Shahada ya Uzamili ya Sheria (LLM), na Shahada ya Uzamivu (Ph.D.) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pamoja na Stashahada ya Uzamili katika Masuala ya Ujumuishaji wa Ulaya kutoka Chuo Kikuu cha Amsterdam.

Dkt. Kibola anatambuliwa kwa mchango wake wa msingi katika kuanzisha taasisi muhimu za kifedha nchini, akiwa Mkurugenzi wa Kwanza wa Huduma za Sheria katika Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Mkurugenzi Mtendaji wa Kwanza wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), na Mkurugenzi Mtendaji Mwanzilishi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja Tanzania (UTT), ambao sasa unajulikana kama UTT AMIS.

Alichukua jukumu la kuongoza uanzishwaji wa DSE kwa kuandaa kanuni za awali za masoko ya mitaji, kuunda mipango ya utekelezaji ya soko la hisa, na kutoa ushauri kuhusu sera muhimu za kisekta. Baada ya kumaliza muda wake katika DSE, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa UTT, ambapo alisimamia uanzishwaji wa mifumo ya uwekezaji wa pamoja na kusaidia kuimarisha mfumo wa kifedha nchini.

Mtazamo wake wa mbali na ujuzi wake katika masuala ya sheria na udhibiti vimeacha alama ya kudumu, na kumfanya kuwa mmoja wa nguzo kuu katika safari ya maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Dkt. Kibola ni Mkurugenzi aliyeidhinishwa na Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania (IoDT), na amewahi kuhudumu katika bodi mbalimbali za taasisi kubwa, zikiwemo Stanbic Bank na Shirika la Bima la Taifa (NIC). Pia ni mwandishi wa machapisho mengi yanayohusu utawala wa kampuni, sheria za biashara, na udhibiti wa masoko ya mitaji.

**Bw. Moremi Marwa - Mkurugenzi wa Bodi**
Moremi Marwa ni kiongozi mahiri wa mashirika, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika utawala wa kampuni, usimamizi wa fedha, na uongozi wa mabadiliko katika sekta za umma na binafsi. Hivi sasa, anahudumu kama Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Kabla ya wadhifa huo, aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Prisons Corporation Sole na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), ambako aliongoza mikakati muhimu ya maendeleo, mipango ya kifedha, na mageuzi ya kidijitali.

Akiwa na rekodi thabiti katika fedha za mashirika, ushirikiano wa kimkakati, na mageuzi ya taasisi, Moremi amecheza nafasi muhimu katika kukuza ukuaji wa taasisi na ufanisi wa kiutendaji. Ni Mhasibu wa Umma aliyeidhinishwa (CPA) na ana Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) katika Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ameboresha ujuzi wake kupitia programu za uongozi katika Harvard Business School, Chuo Kikuu cha Cambridge, na Taasisi ya Aspen.

Sifa zake za kitaaluma zinajumuisha leseni ya kuwa muuzaji wa hisa katika sakafu ya DSE na vyeti vya kitaalam katika uendeshaji wa hazina, ushauri wa uwekezaji, na masoko ya mitaji. Moremi pia amewahi kuwa mjumbe wa bodi mbalimbali, zikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Benki ya Afrika Tanzania, na Strategies Insurance Tanzania, ambako ametoa mwelekeo wa kimkakati na usimamizi wa utawala bora.

Nje ya majukumu yake ya kikampuni, Moremi ni kiongozi wa fikra, akiwa mwandishi mwenza wa vitabu juu ya maendeleo ya kitaifa na uendelezaji wa viwanda, na pia anashiriki katika mijadala ya sera za kifedha kupitia Kamati ya Wataalam wa Sera ya Wizara ya Fedha na Mipango. Uzoefu wake mpana, pamoja na uongozi wake katika masoko ya fedha na utawala wa mashirika, unamfanya kuwa mmoja wa watu muhimu katika kuunda taswira ya kiuchumi na ya kibiashara ya Tanzania.

**Bw. Vinaykant Somaiya - Mkurugenzi wa Bodi**
Bwana Vinaykant Somaiya ni mhasibu aliothibitishwa na Boad ya Wahasibu Tanzania (NBAA). Pia ni Mwanachama wa Taasisi ya Wahasibu Waliothibitishwa na nchi ya Uingereza na Wales. Bwana Somaiya analeta uzoefu wa zaidi ya miongo minne katika uhasibu, kodi, ushauri wa uwekezaji, na utawala wa kampuni.

Alikuwa mshirika (Partner) katika kampuni ya Tanna Somaiya & Co. (1973–1996) na baadae PwC, ambapo alihudumu kama mshirika wa Kitengo cha Kodi na kuchukua majukumu ya kikanda Afrika. Tangu 2006 amekuwa mtaalam mshahuri huru wa kodi na biashara.

Bwana Somaiya amekuwa mkurugenzi kwenye bodi nyingi na kuongoza vitengo mbalimbali , ikiwemo Strategis Insurance Tanzania Ltd (Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji), Alliance Life Insurance Ltd (Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Hatari), Kioo Ltd, Ambase Prospecting Ltd, na Karimjee Jivanjee Foundation (Trustee). Awali, alikuwa Mwenyekiti wa Bodi katika benki ya NCBA na Africaonline Tanzania Ltd.

Uzoefu wake mkubwa katika fedha, kodi, utawala na uongozi unamfanya mchango wake kwenye Bodi kuwa wa thamani sana.

## 5. KAMATI YA UWEKEZAJI

Kamati ya Uwekezaji ndiyo inayoweka mwelekeo wa uwekezaji wa mfuko na kiwango cha hatari kinachokubalika. Inapitisha na kusasisha sera za uwekezaji pamoja na mipaka ya mikopo, ukwasi, na muda wa uwekezaji. Pia inasimamia utekelezaji wa sheria husika na kanuni za mfuko. Kamati hupitia matokeo ya uwekezaji dhidi ya viwango vya rejea, kusimamia washirika wa kifedha, pamoja na mbinu za upangaji bei na uthaminishaji. Masuala yanayojitokeza hushughulikiwa mara moja na mambo muhimu huwasilishwa kwa Bodi.

Vikao hufanyika angalau kila robo mwaka au zaidi kulingana na hali ya soko, na maamuzi yote pamoja na sababu zake huandikwa na kuwasilishwa kwa Bodi kupitia taarifa rasmi.

Kamati hii ina uzoefu mpana katika sheria na udhibiti wa masoko ya mitaji, uongozi wa juu katika soko la hisa na sekta ya mawasiliano, utaalamu wa fedha za kampuni, pamoja na uzoefu wa miongo kadhaa katika uongozi wa biashara na bodi katika benki, bima na viwanda.

| SN | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Dr. Hamisi Kibola (PhD) | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Yogesh Manek | Mjumbe |
| 3. | CPA (T) Moremi Marwa | Mjumbe |

## 6. MENEJIMENT YA MFUKO

**Bw. Mfaume Kimario | Mkurugenzi Mtendaji**

Mfaume Kimario ni mtaalamu mwenye uzoefu wa karibu miaka 20 katika usimamizi wa mifuko ya uwekezaji, masoko, na mawasiliano ya mashirika, akihudumu katika sekta za umma na binafsi. Amejipambanua kwa uwezo mkubwa wa kuunda na kutekeleza mikakati ya masoko, kuongoza timu zenye ufanisi wa juu, na kusimamia mahusiano ya wadau. Katika UTT AMIS, ameongoza miradi kadhaa muhimu ikiwemo uzinduzi wa majukwaa ya kidijitali na utekelezaji wa mikakati ya kimkakati kama sera za mwendelezo wa biashara na mawasiliano ya umma. Uwezo wake wa kuchochea ukuaji wa taasisi kupitia fikra za kimkakati na mawasiliano bora umekuwa msingi wa mafanikio yake.

Msingi wake wa kielimu umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yake ya kitaaluma. Anashikilia Shahada ya Uzamili ya Sera, Usimamizi na Utawala kutoka Chuo Kikuu cha York, Uingereza, yenye msisitizo katika utawala na uundaji wa sera. Pia ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara kutoka Taasisi ya Usimamizi wa Fedha (IFM), yenye mwelekeo wa upangaji wa kifedha na utawala wa mashirika. Shahada yake ya Kwanza ya Sanaa katika Uongozi wa Mashirika kutoka Chuo Kikuu cha Cincinnati ilimpatia ujuzi madhubuti wa kufanya maamuzi na kusimamia timu, huku Stashahada ya Sayansi ya Kompyuta na Teknolojia ya Mifumo ya Taarifa kutoka Cincinnati State ikimuwezesha kupata umahiri katika teknolojia ya habari.

Kwa rekodi iliyothibitishwa ya uongozi, ubunifu, na ushirikishwaji wa wadau, utaalamu wa Kimario wa kimkakati na uwezo wake mpana wa kitaaluma vimekuwa nguzo ya mafanikio ya mabadiliko katika taasisi alizozihudumia. Uwezo wake wa kuunganisha taaluma ya kina na uzoefu wa vitendo unamuweka katika nafasi ya kipekee ya kuongoza katika mazingira changamano na kuleta matokeo yenye athari chanya.

**Bi. Naomi Mfwiri I Meneja wa Biashara na Masoko.**
Naomi ni Meneja wa Mauzo na Masoko ya Biashara katika Africa Pension Fund Limited. Anaongoza juhudi za kuvutia wateja wapya, kukuza ushirikiano wa kimkakati, na kutekeleza mikakati ya ukuaji inayolenga kuongeza ushawishi wa Mfuko sokoni. Akiwa na uzoefu mpana katika masuala ya fedha na usimamizi wa miradi, Naomi aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Masoko ya Fedha (ACI Financial Markets Association). Anachanganya uwezo wa uchambuzi na uelewa wa kibiashara katika kubaini fursa, kujenga mahusiano ya taasisi, na kuongeza mapato kwa njia endelevu. Anachukua jukumu muhimu katika kuweka bidhaa za APeF kwenye nafasi imara ndani ya sekta ya fedha ya Tanzania kupitia ushirikiano wa karibu na wawekezaji wa taasisi, mifuko ya pensheni na wadhibiti.

Naomi ana Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Miradi kutoka Taasisi ya Usimamizi ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI) alikopata matokeo ya juu, na Shahada ya Kwanza ya Biashara na Usimamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ni mwenye Cheti cha ACI Dealing kutoka Chama cha Masoko ya Fedha, Paris, na amepata mafunzo ya Uongozi wa Watendaji (Executive Coaching) katika Chuo cha Biashara cha Strathmore, Kenya. Utaalamu wake wa kitaaluma na uzoefu mpana unamwezesha kuoanisha maendeleo ya biashara na utekelezaji wa kiutendaji, kuhakikisha bidhaa za APeF zinakidhi viwango vya udhibiti na matarajio ya wawekezaji.

**Bw. Aleck Ngoshani | Meneja wa Uendeshaji**

Bw. Aleck ana uzoefu wa zaidi ya miaka kumi katika usimamizi wa shughuli na miradi, akiwa na uzoefu unaohusisha sekta za benki, huduma za uwekezaji, na miundombinu ya masoko ya mitaji. Amejiunga na Africa Pension Fund Limited (APeF) kama Meneja wa Uendeshaji, akisimamia mifumo ya kiutendaji na taratibu za ndani za shirika kulingana na mahitaji ya ukuaji na matakwa ya kisheria.

Kabla ya kujiunga na APeF, Aleck alishika nafasi muhimu za uongozi katika Benki ya Standard Chartered Tanzania na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Pia ni mwanzilishi mwenza wa kampuni ya Wealthora Company Limited, ambako aliongoza miradi mbali mbali, kama majukwaa ya uwekezaji wa kidijitali na huduma za ushauri wa kifedha.

Kazi yake imekuwa ikilenga kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza ufanisi wa taratibu, na kuimarisha ushirikiano kati ya vitengo mbalimbali ndani ya taasisi. Aleck ana Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) kutoka ESAMI, Cheti cha DSE Floor Trader, Cheti cha Securities Industry kutoka CISI, na Stashahada ya Juu ya Teknolojia ya Habari (IT) kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

**Bw. Emanuel Ferdinand Bariki | Meneja wa TEHAMA**

Bw. Emanuel ana uzoefu wa zaidi ya miaka kumi katika uundaji na uandaaji wa mifumo ya TEHAMA na usimamizi wa miundombinu ya kidijitali katika sekta za benki, huduma za kifedha, na taasisi za umma. Kwa sasa, anahudumu kama Meneja wa TEHAMA katika kampuni ya Africa Pension Fund Limited (APeF), akiongoza juhudi za kuandaa miundombinu ya teknolojia, kukuza mifumo ya ndani, na kuhakikisha utayari wa huduma za kidijitali.

Kabla ya kujiunga na APeF, Emanuel alifanya kazi katika Benki ya Diamond Trust Tanzania na Benki ya I&M, ambapo alihusika katika ukuzaji wa mifumo na uunganishaji wa huduma na mifumo ya kitaifa muhimu. Nafasi zake za awali katika taasisi za umma na binafsi zilimpa uzoefu mpana katika maeneo mbalimbali ya TEHAMA, ikiwemo matengenezo ya mitandao, uundaji wa mifumo, na usaidizi wa kiufundi.

Emanuel ana mchanganyiko mzuri wa ujuzi wa kiufundi na uelewa wa umuhimu kwenye suluhisho salama na imara za kiteknolojia. Mchango wake wa kiutendaji unaendelea kusaidia kufanikisha malengo ya kiteknolojia ya APeF.

**Bi. Salma Sharif | Meneja wa Fedha wa Mpito** Bi. Salma anahudumu kama Meneja wa Fedha wa Mpito katika Africa Pension Fund Limited (APeF), akitoa uongozi wa vitendo katika kitengo cha fedha huku akimuunga mkono Afisa Mtendaji Mkuu na Bodi katika masuala ya utawala wa kifedha, uadilifu wa taarifa za fedha, na utii wa kisheria na udhibiti. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka kumi katika ukaguzi, usimamizi wa hatari, utii wa kanuni, na usimamizi wa fedha, akichanganya umahiri wa kitaalamu na utekelezaji wa vitendo ili kuimarisha nidhamu na udhibiti wa kifedha.

Katika nafasi hii ya mpito, Salma anasimamia shughuli za kifedha, upangaji wa bajeti, usimamizi wa mtiririko wa fedha, na utoaji wa taarifa za kifedha, huku akihakikisha ulinganifu na mifumo ya utawala na matakwa ya kisheria. Ana jukumu la msingi katika kuhakikisha maamuzi ya kifedha yana ushahidi wa kutosha, mifumo ya udhibiti inafanya kazi ipasavyo, na mahitaji ya udhibiti wa CMSA na TRA yanatimizwa kikamilifu. Mtazamo wake ni wa kimfumo, wa vitendo, na unaolenga matokeo, ukisisitiza uwajibikaji, uwazi, na utayari wa kiutendaji katika shirika zima.

Salma ana Shahada ya Sanaa katika Uhasibu na Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Coventry, Uingereza.

.

**Bw. Kelvin Michael Nshangeki | Afisa wa Uwekezaji**

Bw. Kelvin ni Afisa Uwekezaji katika Africa Pension Fund Limited (APeF), akihusika katika utafiti wa masoko, ushauri wa uwekezaji, na upangaji wa mikakati ya uwekezaji. Ana uzoefu katika uchambuzi wa hisa, tathmini za kiuchumi, na utoaji wa ushauri kwa wateja.

Kabla ya kujiunga na APeF, Kelvin alifanya kazi kama Mchambuzi wa Utafiti katika kampuni ya Zan Securities, ambapo alitekeleza uchambuzi wa masoko, kuandaa mifano ya tathmini ya thamani ya kampuni, na kusaidia katika kukuza masoko ya mitaji nchini. Pia alihusika katika ushauri wa utoaji wa hati fungani na kuchangia katika kuanzishwa kwa Mfuko wa kwanza wa uwekezaji wa binafsi usio na kikomo nchini Tanzania.

Kelvin pia amewahi kufanya kazi katika nyanja za ukaguzi na ushauri wa kodi. Ni mtaalamu aliyeidhinishwa wa Financial Modelling and Valuation Analyst (FMVA) na mtahiniwa wa kiwango cha tatu cha CFA (Chartered Financial Analyst). Anafanya kazi zake kwa weledi, uchambuzi wa kina, na malengo ya uwekezaji endelevu.

## 7. MAJUKUMU YA MENEJA WA MFUKO

**Meneja wa mfuko atawajibika kufanya yafuatayo:**

a) Kusimamia mfuko kwa mujibu wa waraka wa makubaliano kwa maslahi ya wenye vipande na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria;
b) Kuhifadhi na kuhakikisha kuwa vitabu vya hesabu na kumbukumbu za Mfuko vinahifadhiwa ipasavyo, pamoja na kuandaa hesabu na ripoti za Mfuko;
c) Kuchapisha na kusambaza angalau ripoti mbili za mahesabu kwa mwaka kwa wenyevipande;
d) Kuhakikisha kuwa rejista ya wenyevipande wa mfuko inahifadhiwa na kuhuwishwa wakati wote;
e) Kuwasilisha kwa mtoa bima takwimu sahihi;
f) Kulipa fedha zilizokusanywa kama sehemu ya bei ya ununuzi ya hati ya bima kwa mtoa bima;
g) Kupokea na kuwasilisha madai ya wenyevipande kwa mtoa bima;
h) Kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mtoa bima kabla ya kufanya mabadiliko ya kimuundo katika mfuko;
i) Kushirikiana kikamilifu na mtoa bima au mtu yeyote aliyeteuliwa naye katika uchunguzi, urekebishaji, utatuzi au utetezi wa madai ya bima;
j) Kuandaa mkutano wa mapitio ya hati ya bima ya mwaka na mtoa bima;

k) Kuhakikisha kuwa mkataba wa mdhamini unapatikana kwa umma nchini Tanzania kwa ajili ya ukaguzi bila malipo wakati wote wa saa za kazi katika ofisi za Meneja, na kutoa nakala za nyaraka hizo kwa gharama ya ada ya kawaida.

## 8. MTOA BIMA WA MFUKO WA ZIADA

a) Kampuni ya Alliance Life Assurance ni kampuni iliyosajiliwa nchini Tanzania kwa namba ya usajili 73479 ambae ni mtoa bima chini ya mfuko huu.

b) Bodi ya wakurugenzi wa alliance life assurance limited.
Bodi ya Wakurugenzi inaundwa na watu wafuatao:

| SN. | JINA | CHEO | URAIA |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Shaffin Jamal | Mwenyekiti | Mtanzania |
| 2. | Bw. Yogesh Manek | Mkurugenzi | Mtanzania |
| 3. | Bw. Vinaykant Somaiya | Mkurugenzi | Mtanzania |
| 4. | Bw. Pulin Manek | Mkurugenzi | Mtanzania |
| 5 | Bw. Mohammed Kassongo | Mkurugenzi | Mtanzania |

c) Majukumu ya mtoa bima
Mtoa bima chini ya mfuko huu atawajibika ifuatavyo:

i. Kuandaa hati inayodhibiti bima ya mfuko huu;

ii. Kuhifadhi taarifa zinazohusiana na hati ya bima zinazodhibitiwa chini ya mfuko huu kama inavyotolewa na meneja wa mfuko;

iii. Kuwajibika na kulipa madai yote ya bima kulingana na masharti ya hati ya bima;

iv. Kufanya tathmini ya kila mwaka ya hati ya bima ya mfuko;

v. Kutoa ushauri kwa meneja wa mfuko kuhusu mpango wa bima wa mfuko huu;

vi. Kumjulisha meneja wa mfuko kama kutatokea mabadiliko makubwa katika taratibu za usimamizi wa madai ya bima, wafanyakazi au mikataba ya bima inayoweza kuathiri mfuko.

## 9. MDHAMINI WA MFUKO WA ZIADA

a) **Katiba ya msimamizi ya mfuko**
Mdhamini wa mfuko ni Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo ni benki ya biashara yenye leseni ya kuendesha shughuli za kibenki chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991. Ilianzishwa rasmi tarehe 23 Septemba 1997 na ina Cheti cha Usajili namba 32700. Benki hii inamilikiwa na Absa Group Limited kwa asilimia 55%, pserikali ya Tanzania kwa asilimia 30% na IFC kwa asilimia15%. Ofisi kuu ya benki hii ipo Barabara ya Sokoine, Kivukoni, Dar es Salaam, Tanzania.

b) **Bodi ya wakurugenzi ya mhifadhi wa mfuko**
Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC)inaundwa na watu wafuatao:

| SN. | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Dkt. Elirehema Doriye | Mwenyekiti wa Bodi |
| 2. | Bw. Harish Bhatt | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Bw. Heman Shah | Mjumbe wa Bodi |
| 4. | Bw. Mrisho Yassin | Mjumbe wa Bodi |
| 5. | Bw. Louis Adande | Mjumbe wa Bodi |
| 6. | Balozi Adadi Rajabu | Mjumbe wa Bodi |
| 7. | Bw. Felix Mlaki | Mjumbe wa Bodi |
| 8. | Bw. Godfrey Malekano | Mjumbe wa Bodi |

c) **Majukumu ya mdhamini wa mfuko**

Mdhamini wa mfuko huu atawajibika kufanya yafuatayo:

i. Kusimamia mali zote za mfuko kwa niaba ya wamiliki wa vipande kwa mujibu wa masharti wa waraka wa makubaliano, na kuhakikisha kuwa fedha taslimu pamoja na mali za mfuko zimesajiliwa kwa jina la mfuko;

ii. Kuwajibika kwa makosa yoyote yaliyofanywa na wakala wake ambae amekabidhiwa mali ya mfuko.

iii. Kusimamia na kuhakikisha kuwa ununuzi, uuzaji na kubatilishwa/kufutwa kwa vipande kunatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya waraka wa makubaliano;

iv. Kuhakikisha kwa uangalifu kwamba mbinu zinazotumika na meneja wa mfuko kupata thamani halisi ya vipande ni za kufaa ili kuhakikisha bei za uuzaji na ununuaji wa vipande zinapatikana kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa m akubaliano;

v. Kutekeleza maagizo ya meneja wa mfuko kuhusu uwekezaji kulingana na masharti ya mkataba wa makubaliano;

vi. Kuhakikisha kuwa viwango vya uwekezaji na kukopa kama ilivyoorodheshwa kwenye waraka wa makubaliano na matakwa yaliyoainishwa katika sheria na taratibu zingine zinazohusu uendeshaji wa mfuko huu zinafuatwa;

vii. Kutoa ripoti kwa wamiliki wa vipande itakayojumuishwa katika ripoti ya mwaka ikieleza kwa maoni ya mdhamini wa mfuko, Meneja wa mfuko ameendesha mfuko huu kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa makubaliano. Na kama meneja wa mfuko hajatimiza hivyo, ielezwe hatua gani zilizochukuliwa na mdhamini wa mfuko;

viii. Kuchukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa hatimiliki hazitolewi mpaka malipo kamili yamefanyika na kuthibitishwa na meneja wa mfuko;

ix. Kuhakikisha kuwa hati mbalimbali za uwekezaji zilizoshikiliwa kwa niaba ya wamiliki wa vipande wa mfuko huu zimesajiliwa kwa jina la mfuko;

x. Pale ambapo umiliki wa uwekezaji umehifadhiwa kwa njia ya kielektroniki, basi Meneja wa mfuko atahakikisha rasilimali hizo zinawekewa utaratibu wa kumbukumbu tofauti na mali za Meneja wa mfuko;

## 10. WATU WANAOHUSIANA

Mdhamini, Mtoa Bima, na Meneja si watu waliounganishwa kwa njia yoyote, isipokuwa kwamba Bwana Yogesh Manek, Bwana Shaffin Jamal na Bwana Vinaykant Somaiya ni wakurugenzi wa APeF pamoja na Alliance Insurance.

## 11. RATIBA YA TOLEO

Ratiba ya mauzo ya awali ya hisa za mfuko wa uwekezaji wa pamoja wa Ziada (Ziada Fund) kwa umma ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Mauzo ya awali | 26 Januari 2026 |
| Kufunga Mauzo ya Awali | 25 Februari 2026 |
| Kuanzishwa kwa Hati ya Bima | 26 Januari 2026 |
| Taarifa za Matokeo | 09 Machi 2026 |

**Kumbuka: Katika hali yoyote ile, muda wa Mauzo ya Awali hautaongezwa.**

## 12. TAMKO LA UZINGATIAJI WA SHERIA KUTOKA KWA MENEJA WA MFUKO

Imethibitishwa kwamba:

a) Waraka wa Toleo uliotumwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) umeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 kama iliyorekebishwa na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifumo ya Uwekezaji wa Pamoja) za mwaka 1997.
b) Mahitaji yote ya kisheria yanayohusiana na uzinduzi wa mfuko wa ziada (Ziada Fund), pamoja na miongozo, maagizo, n.k., yaliyotolewa na Serikali na mamlaka nyingine husika, yamezingatiwa kikamilifu.
c) Maelezo yaliyotolewa katika waraka wa toleo ni ya kweli, haki, na ya kutosha ili kuwawezesha wawekezaji kufanya maamuzi ya kuwekeza kwa ufahamu kamili kuhusu mpango unaopendekezwa.

________________________

**Mfaume Kimario,**

**Mkurugenzi Mtendaji**
Dar es Salaam

## 13. GHARAMA ZA AWALI ZA UUZAJI WA VIPANDE

Zifuatazo ni Gharama za awali za uuzaji wa vipande:

- Gharama za matangazo, uchapishaji na shughuli za masoko
- Kamisheni zitakazolipwa kwa mawakala
- Gharama za posta na gharama nyingine ndogo ndogo
- Gharama nyinginezo zinazohusiana na uuzaji wa vipande.

Gharama hizi zitabebwa na Kampuni ya Africa Pension Fund Limited (APeF) Tanzania, ambae ndio Meneja wa Mfuko. Gharama hizo hazitatozwa kwa Mfuko, na hivyo basi hakuna ada ya kujiunga na Mfuko.

## 14. HATARI ZA UWEKEZAJI

Wawekezaji wanapaswa kutambua kwamba uwekezaji katika mfuko huu unahusiana na athari za uwekezaji katika soko, na Thamani Halisi ya Vipande (Net Asset Value) ya mfuko inaweza kupanda au kushuka kulingana na mambo mbalimbali yanayoathiri soko la kifedha. Ufanisi wa awali si lazima uwe kiashiria cha matokeo ya baadae. Wawekezaji wanapaswa kufahamu mambo yafuatayo:

a) Mfuko unawekeza katika hati za serikali, hati fungani zinazotolewa na Taasisi za kibiashara na uwekezaji wa ndani ya nchi zinaweza kukumbwa na hatari ya kushindwa kuhudumia deni au kulipa deni; au kushushwa hadhi na mashirika ya ukadiriaji wa ubora wa kifedha.
b) Mabadiliko ya viwango vya riba yanaweza kuathiri thamani za mapato ya kudumu ambapo mfuko umewekeza.
c) Mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha za kigeni hayawezi kuathiri mapato ya mfuko kwa kuwa mfuko unawekeza kwa kutumia shilingi za kitanzania tu.
d) Mfumo wa kodi unaohusiana na mfuko wa uwekezaji wa pamoja (unit trusts) unaweza kubadilika na hivyo kuathiri mapato ya mfuko.

e) Mabadiliko yoyote katika sheria/miongozo yanaweza kuwa na athari kwa uendeshaji wa mfuko.
f) Vilevile, mambo mengine yasiyotabirika yanaweza kuathiri uwekezaji ambapo ‘Mfuko wa Ziada‘ imewekeza na hivyo kuathiri thamani ya vipande vya mfuko wa Ziada .
g) Wenye vipande kutaka kutoka kwa wingi na kwa wakati mmoja kunaweza kuathiri mfuko.

Mfuko umejidhatiti kuepuka athari hizo zilizotajwa hapo juu kwa kuweka mikakati thabiti ya kuzuia kabisa athari hizo au kuzipunguza kwa kiasi kikubwa.

## 15. TAARIFA ZA MFUKO

**MFUKO WA UWEKEZAJI WA PAMOJA – ZIADA FUND.**

**MADHUMUNI YA MFUKO:** Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja unaounganishwa na bima (Ziada Insurance-Linked Unit Trust Scheme) umeundwa ili kuendana na mahitaji ya kifedha yanayobadilika badilika. Kadri ndoto na matarajio yetu yanavyoongezeka, ndivyo mahitaji yetu ya ulinzi, uwekezaji, na upatikanaji wa fedha yanavyoongezeka katika hatua mbalimbali za maisha. Mpango huu unatoa faida pacha , ikisaidia wawekezaji kufanikisha ukuaji wa mitaji pamoja na bima ya ulinzi unaohakikisha usalama wa kifedha kwa familia zao.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA:** Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa Soko la Fedha unaounganishwa na bima unakuja na vipengele vingi vinayomruhusu mwekezaji kufaidika na Bima na Uwekezaji. Mpango huu unamruhusu kila mshiriki kuunda mpango thabiti wa udhibiti wa kifedha na akiba kwa ajili yake binafsi na familia yake.

**FAIDA ZA BIMA ZITOLEWAZO NA MFUKO:** Mpango huu Bima ya Maisha (ikijumuisha kifo na Ulemavu wa Kudumu) pamoja na gharama za mazishi.

## 16. MALENGO YA MFUKO

a) Kuwezesha jamii ya wawekezaji kuwa na tabia ya kujiwekea akiba na pia kutoa fursa ya kupata ongezeko la thamani ya muda mrefu ya uwekezaji wao.
b) Kutoa faida za bima;.
c) Kuongeza uelewa wa umuhimu wa bima ya maisha nchini.

## 17. WAWEKEZAJI WANAOSTAHILI KUWEKEZA

Mtanzania mkazi wa Tanzania asiye mkazi pamoja na watu binafsi na wasio watu binafsi wanaweza kujiunga na Mfuko huu.

## 18. KIASI CHA UWEKEZAJI

a) **Kima cha chini cha uwekezaji** ni shilingi 50,000; na
b) Shilling 10,000 kwa uwekezaji wa unaofuata/baadae.
c) **Kiasi cha Juu cha uwekezaji** - Hakuna Kikomo (ila Bima ya Maisha ina ukomo wa Shilingi 100,000,000 tu).

**Kumbuka: Mwekezaji anaweza kuwekeza kiasi chochote apendacho ila mradi kima cha chini kiwe shilling 50,000.**

## 19. BEI YA KIPANDE

a) Mauzo ya Awali - vipande vitauzwa kwa Thamani ya Awali ya shilingi 100 kwa kipande (Hii ni kwa sababu gharama za awali za Mfuko zitagharamiwa na Meneja).
b) Mauzo ya Baadae - Vipande vitauzwa kwa Thamani Halisi ya kipande (NET ASSET VALUE) ya wakati huo bila ada ya kuingia kwenye Mfuko.

**Kumbuka: Mfuko utakuwa wazi kwa shughuli za uuzaji na ununuzi wa vipande baada ya siku 10 za kazi kuanzia tarehe ya kufungwa kwa mauzo ya awali.**

## 20. ADA YA KUINGIA

Hakuna ada ya kuingia kwenye mfuko. Vipande vitatolewa/kugawanywa bila kutozwa ada yoyote ya kuingia.

Mauzo ya Baadae - Vipande vitauzwa kwa Thamani Halisi ya kipande (NET ASSET VALUE) ya wakati huo bila ada ya kuingia kwenye mfuko.

## 21. UKWASI/ KUUZA VIPANDE

Moja ya malengo ya mfuko ni kuwa na ukwasi wa kutosha muda wote, ili mwekezaji akitaka kutoka kwenye mfuko apate pesa zake ndani ya wakati, na lengo hili litatekelezwa kwa misingi ifuatayo:

a) Badaa ya mauzo ya awali, uuzaji wa vipande utakuwa wazi kwa kipindi chote baada ya kipindi cha siku 10 za kazi kuanzia tarehe ya kufungwa kwa mauzo ya awali.
b) Meneja wa mfuko atahakikisha maombi ya uuzaji wa vipande yanalipwa ndani ya siku 3 za kazi baada ya kupokea maombi hayo.

**Kumbuka**:

a) Mapato ya uuzwaji wa vipande yatawekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mwekezaji husika au kupitia ya mitandao ya simu.
b) Wawekezaji wanaweza kutuma maombi ya kuuza vipande vyao kwa njia ya kielektroniki kwa kutuma form ya kuuza vipande iliyosainiwa au barua ya maombi, mradi tu kama hakutakuwa na mabadiliko ya taarifa za akaunti ya benki iliyosajiliwa katika daftari la wamiliki wa vipande linalosimamiwa na Meneja.
c) Ukomo wa kiasi cha kuuza kwa mwekezaji mmoja: Meneja ana haki ya kuweka ukomo wa Shilingi 1,000,000,000 kwa siku kwa mwekezaji mmoja wa vipande.Hatua hii inahitajika ili kudumisha ukwasi wa mfuko.

## 22. FAIDA (FAO) ZA BIMA KATIKA MFUKO WA ZIADA

Faida ya bima inapatikana kwa mujibu wa hati ya bima ya maisha ya makundi, Ulemavu wa Kudumu pamoja na bima ya mazishi, kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

| BIMA YA MAISHA | |
|---|---|
| Kiwango cha juu cha bima: 50% yaNAV TZS 250,000- TZS 100,000,000 | |
| **JINA LA MFUKO** | Ziada Insurance-Linked Unit Trust Scheme |
| **Kiwango cha chini cha uwekezaji ili kunufaika na Bima** | TZS 250,000 |
| **Kiwango cha juu ili kunufaika na bima** | TZS 100,000,000 |
| **Ada ya Bima kwa asilimia ya thamani ya vipande.** | 0.25% kwa mwaka |
| **Utaratibu wa Malipo ya Michango ya Bima** | Kila mwaka |
| **Faida za Bima:** | **Kifo na Ulemavu kwa mwenye vipande, Mazishi: Watoto wa mwekezaji** |
| **Kiasi cha Faida Kinacholipwa kwa Kifo au ulemavu wa kudumu** | |
| FAO LA GHARAMA YA MAZISHI | |
| Thamani Vipande | Faida ya Mazishi: mwisho watoto wanne |
| **TZS 5,000,000 – TZS 9,999,999** | **TZS 250,000** |
| **TZS 10,000,000 – TZS 19,999,999** | **TZS 300,000** |

| | |
|---|---|
| **TZS 20,000,000 – TZS 29,999,999** | **TZS 350,000** |
| **TZS 30,000,000 – TZS 49,999,999** | **TZS 400,000** |
| **TZS 50,000,000 – TZS 74,999,999** | **TZS 500,000** |
| **TZS 75,000,000 – TZS 99,999,999** | **TZS 750,000** |
| **NAV> TZS 100,000,000** | **TZS 1,000,000** |

**Kumbuka Masharti ya Bima:**

a) Malipo ya Bima yanatakiwa kulipwa mwanzo wa mwaka husika.
b) Umri unaostahili wa kuingia kwenye bima kuanzia miaka 18 hadi 60
c) Watoto watakaonufaika na bima ni wale wenye umri wa miaka 0 hadi 21 kwa kila mtoto hadi kufikia watoto 4.
d) Kwa wale wenye umiliki wa pamoja (joint life 2) faida zitagawanywa sawasawa
e) Faida za bima zitaanza baada ya miezi 6 isipokuwa ajali tu.
f) Ikiwa mwekezaji ana akaunti za vipande zaidi ya moja basi, kiwango cha juu cha fao la bima kitafikia ukomo wa Shilingi 100,000,000 tu.
g) Kiasi cha fao la kifo na ulemevu wa kudumu, kitakuwa kiwango cha chini kati ya takwimu hizi mbili: kati ya 50% ya thamani ya vipande vya mwekezaji wakati wa kifo au 50% ya wastani wa thamani ya vipande vya siku 30 kabla ya tarehe ya kifo.
h) Fao la gharama za mazishi itapatikana kwa kutumia kiwango cha chini kati ya takwimu hizi mbili: kati ya 50% ya thamani ya vipande vya mwekezaji wakati wa kifo au 50% ya wastani wa thamani ya vipande vya siku 30 kabla ya tarehe ya kifo.
i) Masharti mengine ya kawaida ya sera ya kampuni ya Alliance Life Assurance Ltd yatatumika.

## 23. MASHARTI NA VIGEZO VYA BIMA

a) Umri unaostahiki wa kuwa na bima ni miaka 18 hadi 60 kwa mwekezaji.
b) Umri unaostahiki kwa mtoto wa kuzaa ni kati ya miaka 0 hadi 21.
c) Kwa taasisi, bima itatambua wawakilishi 2 wa taasisi.
d) Faida za bima zitaanza baada ya miezi 6 isipokuwa ajali tu.
e) Iwapo mtu aliye na bima ana akaunti kadhaa ambazo jumla ya thamani halisi ya vipande vyake vinazidi shillingi 100,000,000, basi kiwango cha juu cha fao la bima kitafika ukomo wa Shilingi 100,000,000 tu.
f) Iwapo mwenye bima ana akaunti kadhaa, manufaa ya mazishi yatakayolipwa yatazingatia jumla ya thamani halisi ya vipande vyote.
g) Wenye vipande vyenye thamani ya chini ya shilingi 250,000 hawatalipwa bima.
h) Wenye vipande vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi 100,000,000 , basi fao la bima litalipwa hadi kufikia ukomo wa shilingi 100,000,000 na sio zaidi.

## 24. FAIDA YA GHARAMA ZA MAZISHI

a) Inapatikana kwa wawekezaji wanaostahili ambao watajiunga na mfuko na kutimiza vigezo
b) Faida ya gharama za mazishi itatolewa kwa kiwango cha shilingi 250,000 hadi shilingi 1,000,000 kulingana na thamani halisi ya vipande.

## 25. UTARATIBU WA FAO LA BIMA

| SN | KUTOKEA KWA TUKIO | FAIDA ZA BIMA | | |
|---|---|---|---|---|
| | | MAISHA | ULEMAVU WA KUDUMU NA KAMILI | MAZISHI |
| 1. | Kifo cha Mwekezaji wa vipande | Ndio | Hapana | Hapana |
| 2. | Ulemavu wa Kudumu - kutokana na ugonjwa au ajali | Hapana | Ndio | Hapana |
| 3. | Kifo cha mtoto wa mwekezaji vipande | Hapana | Hapana | Ndio |
| 4. | Kifo cha mwekezaji au mwenza wake | Hapana | Hapana | Hapana |

## 26. FAO LA BIMA - WAKATI WA KIFO

Iwapo mwekezaji wa vipande atafariki, basi mrithi halali atastahili kupokea manufaa yafuatayo:

a. Thamani ya vipande vyote vilivyopo kwa bei ya kipande ya wakati huo- Italipwa na mfuko;
b. Kiasi kinachostahiki cha Bima ya Maisha – Kitalipwa na mtoa bima.

Iwapo mtoto wa mwekezaji wa vipande atafariki kwa bahati mbaya, basi mwekezaji wa vipande atastahili kupokea kiasi kinachostahili cha gharama za mazishi (Kutegemeana na thamani halisi ya vipande) – Itatolewa na mtoa bima.

## 27. FAO - KWA ULEMAVU KAMILI NA WA KUDUMU

Iwapo mwekezaji wa vipande atapata ulemavu wa kudumu kutokana na ugonjwa au ajali wakati wa uwekezaji astahili kupokea :

a. Thamani ya vipande vyote vilivyopo kwa bei ya kipande ya wakati huo - Italipwa na mfuko;
b. Kiasi kinachostahili cha bima ya maisha – Kitalipwa na mtoa bima.

## 28. WAJIBU WA MENEJA KUSHUGHULIKIA MADAI YA BIMA

Madai yote ya bima yatashughulikiwa na mtoa bima kupitia kwa Meneja wa Mfuko. Katika tukio la kifo/ulemavu wa kudumu wa mwekezaji wa vipande, mlezi/mrithi halali anaweza kuwasilisha madai na kuambatanisha nyaraka zote muhimu na sahihi. Madai yote ya bima yatalipwa ndani ya Jamuhuri ya Muungano Tanzania na malipo yatatolewa kwa Shilingi za Kitanzania tu.

## 29. MASHARTI YA KUINGIA KWENYE MFUKO

Kila mwekezaji anayestahili kushiriki katika mfuko atalazimika:

a) Kujaza fomu ya maombi kamili kama ilivyobainishwa na meneja
b) Kulipia kiasi kinachohitajika kupitia njia za malipo kama zilivyoainishwa kwenye fomu ya maombi.

**Kumbuka: Fomu zinaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya APeF: www.apef.co.tz**

## 30. MALIPO YA KIWANGO CHA BIMA

a) **Kiwango Cha Bima**
   i. Kulingana na masharti ya mfuko, kiwango cha bima kinatakiwa kulipwa na wenye vipande (kupitia meneja) kwa mtoa bima ili kupata manufaa mbalimbali ya bima yanayopatikana chini ya hati ya bima ya maisha ya kikundi, ulemavu wa kudumu, na bima ya mazishi.
   ii. Hata hivyo, inapaswa kuzingatiwa kwamba wawekezaji wa vipande watakaojiunga na mfuko wakati wa mauzo ya awali, kiwango cha bima cha mwaka wa kwanza kitalipwa

na Meneja (Africa Pension Fund), na hivyo vipande vitagawanywa kwa kiasi kamili cha maombi ya mauzo ya awali.

iii. Kiwango cha bima kinalipwa kama asilimia halisi ya Thamani Halisi ya vipande kwa kila mwaka, ikizingatiwa kikomo cha juu cha Thamani Halisi ya vipande cha shillingi 100,000,000 – ikimaanisha kwamba kwa wawekezaji ambao Thamani Halisi ya vipande vyao inazidi shillingi 100,000,000, malipo ya kiwango cha bima kwa kila mwaka yatazingatia kikomo cha juu cha shillingi 100,000,000 tu.

iv. Kiwango cha bima kinalipwa kama asilimia halisi ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) kwa kila mwaka, ikizingatiwa kikomo cha chini cha Thamani Halisi ya vipande ya shillingi 250,000 – ikimaanisha kwamba kwa wawekezaji ambao Thamani Halisi ya vipande vyao iko chini ya shillingi 250,000, hawa hawatalipa gharama za bima.

v. Kwa sasa, kiwango cha malipo ya kila mwaka cha Bima kimebainishwa kama ifuatavyo:

| SN | CHAGUO LA UWEKEZAJI | Kiwango cha Michango ya Bima (kinalipwa kila mwaka kwa Mtoa Bima) |
|---|---|---|
| 1. | Thamani halisi ya vipande (NAV) | 0.25% ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) ikizingatiwa kikomo cha juu cha shillingi 100,000,000 na kikomo cha chini cha shilingi 250,000. |

vi. Kiasi kilichobaki (yaani, kiasi cha uwekezaji ukitoa kiwango cha bima) kitatumika kugawa vipande kwa wawekezaji, kwa Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) iliopo.

vii. Kiwango cha bima kinalipwa kwa mtoa bima kutoka kwa uwekezaji wa baadae unaofanywa na mwekezaji katika mfuko.

viii. Kiwango cha bima kinaweza kubadilishwa na meneja akikubaliana na mtoa bima. Tafadhali rejea kifungu cha mapitio katika sera ya bima ya kikundi. Mabadiliko ya kiwango cha bima (ikiwa yatatokea) yatakuwa chini ya masharti yafuatayo:
- Notisi ya miezi miwili ya mabadiliko yaliyokusudiwa ya kiwango cha bima itolewe kwa wawekezaji; na
- Wawekezaji waruhusiwe kujitoa katika mfuko wakati wa kipindi cha taarifa kwa Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value).

**Jedwali la Malipo ya Bima (Hulipwa Kila Mwaka kwa Mtoa Bima): Mfano:**

| Thamani halisi ya Vipande | Gharama ya Bima (% of Net Asset Value) | Gharama za Bima (Premium) |
|---|---|---|
| **1,000,000** | **0.25% ya kiasi cha uwekezaji wako Kumbuka: kiwango cha juu cha shillingi Millioni 100.** | **2,500** |
| **2,000,000** | | **5,000** |
| **3,000,000** | | **7,500** |
| **4,000,000** | | **10,000** |
| **5,000,000** | | **12,500** |
| **10,000,000** | | **25,000** |
| **20,000,000** | | **50,000** |
| **25,000,000** | | **62,500** |
| **30,000,000** | | **75,000** |
| **50,000,000** | | **125,000** |
| **100,000,000*** | | **250,000** |
| **200,000,000*** | | **250,000** |

**(*) Endapo Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) inazidi shilingi 100,000,000/=, kiwango cha bima kitatolewa kwa kikomo cha juu cha shillingi 100,000,000/= tu.**

## 31. RATIBA YA MALIPO YA KIWANGO CHA BIMA

a) **Mauzo ya awali ya vipande**

| Shughuli | Tarehe ya malipo ya kiwango cha Bima | Tarehe ya mwisho ya Malipo ya kiwango cha Bima |
|---|---|---|
| Wawekezaji wakijiunga na mfuko wakati wa mauzo ya awali. | Tarehe ya kutangaza matokeo ya mauzo ya awali | Ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya kutangaza matokeo ya mauzo ya awali. |

b) **Mauzo ya baadae**

Malipo ya kiwango cha bima kwa wawekezaji kwa kila mwaka yatafanyika kabla ya kumalizika kwa siku ya pili ya mwezi unaofuata.

**Kumbuka: Wakati wa kipindi cha mauzo ya baadae, malipo ya bima kwa mtoa bima yatalipwa kwa tarehe maalum (kila mwezi) itakayobainishwa kuanzia tarehe ya kufungwa kwa mfuko.**

## 32. KIFUNGU CHA MAPITIO CHA HATI YA BIMA YA KIKUNDI

Kifungu cha mapitio kimeingizwa katika hati ya bima ya kikundi. Kifungu hiki kitatoa fursa kwa pande zote mbili (yaani, wawekezaji wa vipande na mtoa bima) kupitia jinsi hati ya bima ilivyotekelezwa katika mwaka uliotangulia wa bima. Kifungu hicho cha mapitio kinalenga hasa kufanikisha mambo yafuatayo:

a) Inamruhusu mtoa bima kukagua hali halisi ya vifo na maradhi katika mwaka husika wa bima na kuilinganisha na makadirio ya awali.
b) Iwapo kutakuwa na mabadiliko yoyote ya kisheria, huu ndio wakati wa kutekeleza mabadiliko hayo.
c) Inamruhusu mtoa bima kukagua muda wa kushughulikia madai na iwapo unalingana na matarajio.
d) Kukagua iwapo makadirio yaliyofanywa katika kipindi husika, mfano malipo ya bima, madai n.k., yalikuwa sahihi na kama kuna marekebisho yanayohitajika kufanywa.
e) Mabadiliko yoyote makubwa katika bima hufanywa katika tarehe ya mapitio.
f) Ni fursa ya kufanya ukaguzi wa utendaji wa hati ya bima.

## 33. UUZAJI WA VIPANDE

a) Uuzaji wa vipande katika kipindi cha mauzo ya awali utafanyika kwa thamani ya awali ya shilingi 100/- kwa kila kipande, na katika kipindi cha mauzo ya baadae uuzaji wa vipande utafanyika kwa kutumia Thamani Halisi ya kipande (Net Asset Value) kwa wakati huo.
b) Vipande vitatolewa mpaka nukta nne za desimali.
c) Uuzaji wa vipande ni mpaka pesa itakapopokelewa na meneja kutambua kiasi kilichowekezwa na kwa kuongezea, baada ya mwombaji kutimiza masharti yote yaliyowekwa chini ya Mfuko kwa madhumuni ya uwekezaji.
d) Taarifa ya akaunti itatolewa baada ya manunuzi ya vipande.

## 34. TAARIFA YA AKAUNTI

a) Baada ya mchakato wa miamala yote, Taarifa ya Akaunti (SOA) itatolewa. Taarifa ya akaunti itajumuisha maelezo kama namba ya akaunti ya mwekezaji, tarehe ya kuanza, maelezo ya miamala, na salio la vipande, kulingana na uwekezaji husika.
b) Mfuko utatoa taarifa ya akaunti ndani ya siku 7 za kazi kuanzia tarehe ya kukubaliwa kwa maombi yanayohusisha ununuzi wa vipande. Hata hivyo, utoaji wa taarrifa kwa

wawekezaji kutokana na ombi lao utatolewa papo hapo baada ya kupokelewa kwa ombi la mwekezaji katika ofisi ya APeF [lakini si zaidi ya siku 7 za kazi].

c) Zaidi ya hayo, taarifa za akaunti zinazohusiana na wamiliki wa vipande watakaojiunga na mfuko wakati wa kipindi cha mauzo ya awali, zitatolewa/kutumwa kama ilivyoainishwa kwenye waraka wa toleo.

**35. UWEKEZAJI NA ZUIO LA MIKOPO**

a) Mfuko huu hauruhusiwi kukopa
b) Sera ya uwekezaji inadhamiria kuwekeza katika hatifungani na bidhaa nyingine katika masoko ya fedha kwa bei halisi ili kufanikisha malengo ya mfuko
c) Sambamba na Sera ya ya uwekezaji, Meneja mfuko hatowekeza mali za mfuko katika hisa.
d) Uwekezaji wa mali za mfuko utatekelezwa kulingana na kanuni zinazotolewa na Mamlaka mara kwa mara sambamba na Sera ya uwekezaji ya mfuko kama iliyoainishwa hapa chini.

**36. SERA YA UWEKEZAJI**

Mgawanyo wa mali katika sera ya uwekezaji wa Mfuko utakuwa kama ifuatavyo:

a) Soko la Fedha: Mfuko unaweza kuwekeza fedha zote kwenye masoko ya fedha bila kuwekeza kwenye hisa
b) Soko la fedha linajumuisha: Hati Fungani za Serikali za muda mrefu, Hati fungani za Serikali za muda mfupi, Hati Fungani za Mashirika, Amana za Benki, Makubaliano ya Ununuzi na Uuzaji (Repurchase agreements), n.k.
e) Mabadiliko katika Muundo wa Uwekezaji: Kulingana na Kanuni za CMSA, muundo wa mgawanyo wa mali ulioainishwa hapo juu unaweza kubadilika, kwa kuzingatia hali ya soko, fursa za soko, kanuni zinazotumika, na vigezo vya kisiasa na kiuchumi. Uwiano huu unaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na mtazamo wa meneja; lengo likiwa daima ni kulinda maslahi ya wamiliki wa vipande. APeF itaarifu mamlaka ndani ya wiki moja kuhusu mabadiliko yoyote katika Muundo wa Uwekezaji.

**Kumbuka: Chini ya sheria za usalama zinazotumika nchini Tanzania, Mfuko - 'ZIADA FUND' hauruhusiwi kukopa.**

**37. UTHAMINI WA MALI ZA MFUKO**

Uthamini wa mali za mfuko utafanyika kila siku ya kazi na thamni yake kutangazwa.

**38. UTEUZI WA MRITHI (NOMINEE)**

a) Huduma ya uteuzi wa mrithi zinapatikana chini ya mfuko;
b) Mwekezaji anaweza kuteua mtu mmoja hata kama ni mtoto akiwa na msimamizi wake ili kumrithi mwekezaji, kama ikitokea mwekezaji atafariki.
c) Wakati wa kunua vipande mwekezaji anaweza kujaza fomu ili kuteua mrithi wake.
d) Uteuzii unaweza kubadilishwa na mwekezaji wa vipande wakati wowote wa uanachama wake;
e) Ikiwa mwekezaji atafariki, basi vipande hivyo vitakuwa mali ya mrithi, baada ya kutimiza taratibu zinazohitajika, fao la kifo litalipwa kwa mrithi.

**Kumbuka: Uteuzi wa mwakilishi unapaswa kufuata masharti mengine ya kisheria. Katika tukio la mzozo kati ya warithi na kesi zinazofuata sheria, zinazosababisha agizo la mahakama linaloelekeza ugawaji wa mali kwa msingi tofauti na ule ulioainishwa kama mrithi, basi agizo la mahakama ndilo litafuatwa na meneja.**

## 39. NJIA ZA UMILIKI WA VIPANDE

Mfuko wa Ziada Fundunaruhusu kumiliki vipande kwa pamoja.

a) Umiliki wa pamoja wa vipande utaruhusiwa, mradi wamiliki wote wa pamoja watatimiza masharti na vigezo vya mfuko.
b) Katika hali ya umiliki wa pamoja, haki zote na stahiki zinazohusiana na mfuko zitatumika kwa pamoja na wamiliki wa pamoja isipokuwa kama makubaliano ya maandishi yamefanywa vinginevyo.

## 40. MUUNDO WA HATI YA BIMA

a) Ulinzi wa bima unaohusishwa na mfuko utatolewa kwa wamiliki wa pamoja wa vipande.
b) Kila mwekezaji wa vipande, atahitajika kuomba fao la bima
c) Fao la bima, ikijumuisha fao la kifo, ulemavu wa kudumu, na fao la mazishi, yataamuliwa kulingana na Thamani Halisi ya vipande ( Net Asset Value).
d) Katika hali ya umiliki wa pamoja wa vipande, stahili kwa kila mwekezaji wa kipande kwa manufaa ya bima kutapimwa kwa kila mwekezaji.

## 41. MASHARTI MENGINE YA BIMA

a) Hati ya bima itamuhusisha mwekezaji wa vipande aliyepewa bima tu na haiwezi kuhamishwa.
b) Manufaa ya bima yatategemea masharti, na vigezo stahili vilivyoainishwa na mtoa bima, ikiwemo umri, vipindi vya kusubiri, na kikomo cha juu cha manufaa.

## 42. DHAMANA YA MKOPO AU KUHAMISHA FAO LA BIMA.

Fao la bima ya mfuko haliwezi kutumiwa kama dhamana ya mkopo au kuhamisha kwa mtu mwingine.

## 43. UWEZO WA KUHAMIA MIFUKO MINGINE

Uhamiaji wa mfuko mmoja kwenda mwengine ikiwa yote inasimamiwa na meneja APeF inaruhusiwa. Uhamisho huu utafanyiwa kazi kwa kuzingatia thamani halisi ya vipande na utafanyika kwa njia ya uuzwaji wa vipande ndani ya mfuko anaotoka (OUT) na kuwekezwa kwenye mfuko anaohamia (IN) kama mwekezaji anakidhi kuwekeza kwenye mfuko huo. Muhimu, mafao ya bima hayataweza kuhamishika wala kupewa mwekezaji mwengine.

## 44. MAOMBI ZAIDI YA MOJA KUTOKA KWA MWEKEZAJI MMOJA

a) Mtu anaweza kuwa mwekezaji katika mfuko huu kupitia ombi moja au zaidi kwa kipindi fulani, ilimradi tu anakidhi umri wa mika 18 mpaka 60;
b) Mwekezaji anayejiunga na mfuko huu zaidi ya mara moja anatakiwa kuhakikisha kuwa namba yake ya utambulisho pamoja na jina la mrithi ni sawa katika maombi yote aliyoyafanya ndani ya mfuko huu kama mtu mmoja;

**Kumbuka: Wawekezaji wa vipande wanaofanya maombi zaidi ya moja kwa kutumia vitambulisho tofauti na/au majina tofauti ya warithi wanapaswa kufahamu kuwa, endapo mwekezaji huyo atafariki, madai yatazingatia haki zote kutoka kwa maombi hayo yote. Lakini pia, wawekezaji watambue kuwa kuna uwezekano wa manufaa ya bima kukataliwa, jambo ambalo halitakuwa na manufaa kwa warithi waliokusudiwa.**

c) Vilevile, kwa hali kama hiyo, manufaa ya bima yataamuliwa kwa kuzingatia jumla ya thamani ya vipande (Net Asset Value).

## 45. UNUNUZI WA VIPANDE

a) **Lini vipande vinaweza kununuliwa**

Vipande vinaweza kununuliwa katika siku yoyote ya kazi wakati wa kipindi cha mauzo ya awali na/au kipindi cha mauzo yanayofuata [ambacho kitaanza si zaidi ya siku 10 za kazi baada ya kufungwa kwa mauzo ya awali].

Mauzo ya awali ya mfuko yatafanyika kuanzia tarehe 26 Januari 2026 hadi 25 Februari 2026.

**Kumbuka:**

i. Fomu ya maombi ya ununuzi wa vipande pamoja na waraka wa toleo ya Mfuko vinapatikana kwa wawekezaji kupitia tovuti ya APeF: www.apef.co.tz

ii. Wawekezaji wanaruhusiwa kuwasilisha maombi zaidi ya moja wakati wa kipindi cha mauzo ya awali.

b) **Ni wapi vipande vinaweza kununuliwa**

Wakati wa mauzo ya awali na mauzo yanayofuata vipande vya Mfuko wa Ziada vinaweza kununuliwa kupitia mawakala wafuatao walioidhinishwa:

i. Matawi yote ya Benki ya NBC Bank Tanzania
ii. Matawi yote ya Benki ya Exim Bank Tanzania
iii. Matawi yote ya Benki ya Azania Bank Plc
iv. Matawi yote ya Benki ya Mwanga Hakika Bank
v. Matawi yote ya Benki ya CRDB Bank Plc
vi. Matawi yote ya Benki ya NMB Bank Plc
vii. Matawi yote ya Benki ya Coop Bank Tanzania (Benki ya Ushirika)
viii. Ofisi za ma Wakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, wakiwemo:

Tanzania Securities Ltd, Solomon Securities Ltd, TIB Rasilimali Limited, Orbit Securities Co. Ltd, Vertex International Securities Ltd, Core Securities Limited, Zan Securities, E.A Capital Limited, Optima Corporate Finance Limited, Smart Stock Brokers Ltd, Victory Financial Services Ltd, Exodus Advisory, FIMCO Ltd, Global Alpha Capital Ltd, Stanbic Ltd, iTrust Finance Ltd, Yusra Sukuk Co. Ltd, Wealth Capital Fund, LASE Securities Ltd, CRDB Bank Plc and Kadoo Securities Ltd.

i. Manunuzi kupitia njia ya kidigitali:

Iwapo mwekezaji ataamua kununua vipande kwa njia za kidigitali na kupakua fomu ya maombi - tovuti: www.apef.co.tz au Msimbo: ***150*74#** au Programu Tumizi (Mobile Application): **APeF App**.

## 46. MALIPO YA UNUNUZI WA VIPANDE

Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vipande wakati wa mauzo ya awali na mauzo yanayofuata yatafanyika kwa kulipia fedha taslimu kwa shilingi ya Tanzania au kwa hundi ya benki itakayolipwa kwa jina la: "Ziada Collection Account," katika ofisi yoyote kati ya zile zilizotajwa hapo juu.

**Kumbuka: Fedha taslimu au hundi kwa ajili ya ununuzi wa vipande vya mfuko huu havipaswi kupelekwa kwa wakala yeyote isipokuwa katika ofisi zilizotajwa hapo juu.**

## 47. MANUNUZI YA VIPANDE BAADA YA KIPINDI CHA AWALI

Manunuzi ya vipande vya mfuko yataanza baada ya kipindi cha awali, yaani tarehe 09 Machi 2026. Kuanzia tarehe hiyo, mwekezaji atanunua vipande kwa thamani halisi (Net Asset Value). Taratibu za ununuzi wa vipande zitakuwa kama ifuatavyo:

a) Manunuzi ya vipande yatafanyika kwa kuzingatia Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) bila ada yoyote;

b) Wawekezaji wanashauriwa kuangalia Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) ya Mfuko wa Ziada wakati wanafanya uamuzi wa kununua vipande. Ikiwa kuna mashaka, wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na washauri wao wa uwekezaji kwa ushauri wa kitaalamu;
c) Iwapo mwekezaji ataamua kununua vipande, ataweza kufanya hivyo kupitia ofisi za mawakala walioteuliwa hapo juu na kupatiwa fomu na maelekezo ya mfuko.
d) Mwekezaji anapaswa kujaza fomu sahihi ya maombi ya ununuzi wa vipande vya Mfuko wa Ziada.
e) Fomu za maombi zinapaswa kuwasilishwa katika ofisi za wakala mojawapo walioorodheshwa ikiwa imeambatanishwa na aliyeteuliwa kama mrithi, ikiwa na mojawapo ya malipo yafuatayo:
    - Fedha taslimu kwa sarafu ya Tanzania; au
    - Hundi ya benki ya iliyowekewa mstari wa "Not Negotiable," na kulipwa kupitia akaunti ya benki yenye jina "Ziada Collection Account"
f) Maombi ya ununuzi wa vipande baada ya mauzo ya awali yatazingatiwa na kukubaliwa kwa mawakala katika siku yoyote ya kazi na kufanyiwa kazi kama yatakuwa yamepokelewa ndani ya saa za kazi za benki (03:00 asubuhi hadi 10:00 jioni);
g) Maombi yote ya ununuzi wa vipande baada ya mauzo ya awali, yaliyopokelewa na kukubaliwa na mawakala walioidhinishwa na APeF, yatafanyiwa kazi na kuchakatwa kwa kuzingatia thamani halisi ya kipande (Net Asset Value) ya wakati huo;
h) Mkataba wa manunuzi ya ununuzi wa vipande vitengo kutoka APeF utachukuliwa kuwa umekamilika siku husika ya kukubaliwa kwa maombi, isipokuwa pale ambapo maombi yatakuwa yamekataliwa yatakataliwa na meneja wa mfuko;
i) Taarifa za ya akaunti (Statement of Account – SOA) zitatumwa kwa wawekezaji walionunua vipande katika kipindi cha mauzo ya baadae ndani ya siku 7 za kazi.

**48. MIAMALA YA WASHIRIKA**

Africa Pension Fund Ltd Tanzania haitawekeza katika "Mfuko wa Ziada."

**49. MAONI NA MALALAMIKO YA MWEKEZAJI**

Wawekezaji wote wanaweza kuelekeza malalamiko yao kwa:
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Africa Pension Fund Ltd (APeF)**
**S.L.P. 6422, Dar es Salaam**
**Simu ya mezani: +255 22 2600 166**
**Barua pepe: apef@apef.co.tz**
**Tovuti: www.apef.co.tz**

**Kumbuka: Fomu ya *Huduma kwa Mwekezaji/Malalamiko* inapatikana katika ofisi za Africa Pension Fund Limited Tanzania (APEF) au kwa mawakala wake walioteuliwa, pamoja na kwenye tovuti ya APeF: www.apef.co.tz .**

**50. GHARAMA ZA MFUKO**

Kutakuwa na gharama zifuatazo katika Mfuko:

a) Kodi, kwa mujibu wa viwango husika;
b) Kamisheni kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na mamlaka husika kama mamlaka ya mitaji na masoko;
c) Ada ya meneja ambayo ni asilimia 1.60 ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) kwa mwaka;

d) Ada ya mdhamini wa mfuko, ambayo ni asilimia 0.1 ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) kwa mwaka, ikiwa na kiwango cha chini cha shiling 6,000,000/=;
e) Gharama nyingine, ambazo ni asilimia 0.9 ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value), ambazo zinajumuisha gharama za kawaida za uendeshaji kama:
    - Gharama za kuuza pamoja na matangazo
    - Gharama za benki
    - Ada za ukaguzi wa hesabu
    - Ada za huduma za kisheria
    - Gharama za miamala ya usambazaji wa vipande
    - Gharama za kuhudumia wawekezaji, n.k.

Hata hivyo, jumla ya gharama nyingine pamoja na ada ya meneja/ushauri wa uwekezaji hazitazidi asilimia 2.6 ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value). Iwapo gharama nyingine zitazidi asilimia 0.9 ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value), sehemu iliyozidi italipwa na meneja wa mfuko. Gharama zote za kipindi cha mauzo ya awali zitalipwa na meneja, lakini baada ya hapo, gharama zote zitabebwa na mfuko.

**Kumbuka: Taasisi za kibiashara na watu binafsi walio nje ya umri unaostahili wa miaka 18 hadi 60 hawatastahili kupata bima ya maisha na wataondolewa kwenye ada ya bima ya asilimia 0.25 kwa mwaka.**

## 51. UTHAMINI WA THAMANI HALISI YA VIPANDE

Thamani Halisi ya mfuko itapigiwa mahesabu kwa kubaini thamani ya mali za mfuko na kutoa madeni ya mfuko pamoja na makadirio mengine. Thamani Halisi ya kipande itahesabiwa kwa kugawanya Thamani Halisi ya mfuko kwa idadi ya vipande vilivyo tolewa na mfuko hadi siku hiyo ya mahesabu. Mfuko utatangaza Thamani Halisi ya kipande (Net Asset Value) yake ya kwanza ndani ya siku 10 za kazi tangu tarehe ya kufungwa kwa mauzo ya awali, na baada ya hapo thamani hiyo itatangazwa kila siku kama ifuatavyo:

a) Thamani Halisi ya Vipande (Net Asset Value) itatumwa kwa vyombo vya habari kwa ajili ya kuchapishwa kila wiki;
b) Thamani Halisi ya Vipande (Net Asset Value) itachapishwa kwenye magazeti yenye usambazaji mpana nchini Tanzania;
c) Net Asset Value itatolewa kila siku kupitia tovuti ya APeF: www.apef.co.tz;
d) Iwapo katika siku yoyote ya tathmini ya thamani ya vipande itashindwa kufanyika kwasababu, Soko la Hisa la Dar es Salaam limefungwa au kwa sababu ya kuwa ni siku za mapumziko, sikukuu au sababu nyingine yoyote, bei ya siku ya kazi iliyopita itatumika kwa madhumuni ya kupigia mahesabu ya Thamani Halisi ya Vipande wa Mfuko (Net Asset Value);
e) Endapo kutatokea mabadiliko makubwa ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value), kama kupanda au kushuka kwa ±1.5% au zaidi kutoka thamani ya siku ya kazi iliyopita au kasoro yoyote ya bei inayotokana na matukio ya soko au makosa ya tathmini, meneja wa mfuko atawaarifu mara moja wawekezaji wa vipande na taarifa hiyo itatumwa kwa njia ya SMS na/au barua pepe kwa wamiliki wote waliosajiliwa ndani ya saa 24 tangu kugundulika kwa mabadiliko hayo au hitilafu hiyo;
f) Meneja wa mfuko atahifadhi na kudumisha rekodi ya kila siku ya Thamani Halisi ya vipande (Net Asset Value) vilivyoshikiliwa, kutolewa, kuuzwa, kubadilishwa, pamoja na thamani ya jalada la vipande na maelezo yote muhimu yanayohitajika baada ya kila tathmini.

## 52. HAKI NA HUDUMA KWA WAWEKEZAJI WA VIPANDE

a) Wawekezaji wa Mfuko wa Ziada wanayo haki ya uwiano katika umiliki wa mali za mfuko huu.
b) Wawekezaji wa Mfuko wana haki ya kumuuliza meneja (APeF) taarifa yoyote ambayo inaweza kuwa na athari hasi kwa uwekezaji wao, na meneja atawajibika kutoa taarifa hizo kwa wamiliki wa vipande.
c) Muhtasari wa ripoti ya mwaka kuhusu mfuko huu utatolewa kwa wawekezaji ndani ya miezi minne tangu kufungwa kwa mwaka wa hesabu husika, na pia utapatikana katika ofisi ya meneja kwa ajili ya kukaguliwa na wawekezaji.
d) Mwaka wa fedha wa mfuko huu utafungwa tarehe 31 Disemba ya kila mwaka.
e) Mabadiliko yoyote ya sifa za msingi za mfuko huu yatafanyika tu pale ambapo wamiliki wa vipande watapewa nafasi ya kujitoa kwa kuuza vipande vyao kwa thamani halisi (Net Asset Value), pamoja na taarifa binafsi kwa kila mwekezaji na kuchapishwa kwenye magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yenye usambazaji mpana nchini Tanzania.
f) Wamiliki wa vipande wana haki ya kukagua nyaraka zifuatazo bila malipo katika ofisi za APeF:

   i. Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura 79 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   ii. Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko wa Uwekezaji wa Pamoja), 1997 [GN Na. 770 ya mwaka 1997].
   iii. Sheria ya Makampuni, Sura 212 (Sheria Na. 12 ya 2002) ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   iv. Waraka wa Mdhamini (Trust Deed) wa Mfuko wa Ziada.
   v. Waraka wa Toleo (Offer Document) wa Mfuko wa Ziada.

g) Mwekezaji atakuwa na haki ya kutumia vipande vyake katika Mfuko wa Ziada kama dhamana au rehani kwa ajili ya kupata mikopo kutoka kwa Taasisi yoyote ya Fedha iliyopewa leseni

## 53. UHUSIANO KATI YA BEI YA MANUNUZI AU MAUZO NA THAMANI HALISI YA KIPANDE (NET ASSET VALUE - NAV)

a) Bei ambayo kipande kitauzwa au kununuliwa katika siku yoyote ya kazi itapangwa kwa kuchukua Thamani Halisi ya Kipande (NAV) ya siku husika bila kuongeza au kutoa ada yoyote ya huduma. [Inamaanisha kwamba uuzaji na ununuzi wa vipande vyote utafanyika kwa thamani halisi inayotumika kwa wakati huo].

b) Kila uuzaji au ununuzi wa vipande vya Mfuko utakuwa halali kuanzia Tarehe ya Kukubaliwa na malipo yake yatafanyika kwa Thamani Halisi ya Vipande itakayokuwa inatumika.

c) Mfuko utachapisha mapema iwezekanavyo, kila siku ya kazi, bei za uuzaji na ununuzi wa vipande katika magazeti yenye usambazaji mpana, isipokuwa wakati wa Kipindi cha Tulivu "Cool-off" kisichozidi siku 10 za kazi tangu tarehe ya kufungwa kwa mauzo ya awali.

## 54. MAZINGIRA YANAYOWEZA KUFANYA SHUGHULI ZA MFUKO KUAHIRISHWA AU KUFUNGWA

a) Meneja hatafanya uuzaji au ununuzi wa vipande katika Kipindi cha Utulivu "Cool-off", kipindi kisichozidi siku 10 za kazi tangu tarehe ya kufungwa kwa mauzo ya awali.
b) Meneja, kwa idhini ya Mamlaka, atasitisha ununuzi wa vipande endapo kutatokea mazingira ambayo yako nje ya uwezo wake.
c) Meneja ataahirisha hadi siku inayofuata ya kazi ununuzi wa vipande iwapo asilimia 10 ya vipande vitauzwa ndani ya siku moja.

d) Shughuli za Uuzaji na Ununuzi hazitafanywa na Meneja wakati wa kufungwa kwa vitabu vya hesabu.

## 55. KIPINDI KATI YA KUPOKEA OMBI LA UUZWAJI VIPANDE NA MALIPO YA FEDHA

a) Uzwaji vipande utafanyika mara tu Taarifa ya Akaunti itakapopokelewa na Meneja au wakala wake ikifuatana na ombi la uuzwaji au hati nyingine yoyote itakayoidhinishwa na Meneja na kupitishwa na Mamlaka, ikiwa imejazwa kikamilifu kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.
b) Malipo ya mapato ya uuzwaji yatatolewa ndani ya siku 3 za kazi kuanzia tarehe ya kukubaliwa kwa maombi yaliyokamilika kikamilifu na Meneja au wakala wake. Malipo yatafanywa kwa njia ya uhamisho wa benki kwa Wamiliki wa Vipande waliotoa taarifa za akaunti zao kwa Meneja, au kwa njia ya posta au njia ya miamala ya simu za mkononi kwa Wamiliki wa Vipande ambao hawajatoa taarifa za akaunti za benki.

## 56. KODI

Taarifa zilizo hapa chini ni kwa madhumuni ya kutoa taarifa kwa ujumla kwa wanunuzi wa vipande wa Mfuko huu. Kwa kuwa kodi zinatofautiana kwa mujibu wa sheria, tunashauri kila mwekezaji awasiliane na mshauri wake wa kisheria au wa kodi ili kupata ushauri maalum kuhusu athari za kodi zinazotokana na ushiriki wake katika Mfuko huu.
Kwa mujibu wa sheria za kodi zilizopo hadi tarehe ya waraka huu wa toleo, athari za kodi kwa Mfuko huu ni kama ifuatavyo:

a) Mapato ya riba yatokanyo na Mfuko huu yatozwa kodi kwa kiwango cha10% kupitia kodi ya zuio (withholding tax), ambayo ni kodi ya mwisho.
b) Faida za mtaji zinazopatikana kutokana na mauzo au ukomavu wa uwekezaji ulioko kwenye masoko ya fedha na kumilikiwa na Mfuko huu hazitozwi kodi.

## 57. UKOMO WA MFUKO

Mfuko utafikia ukomo kama:

a) Itaamriwa katika mkutano mkuu maalum wa wawekezaji;
b) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana itatumia vipengele 122 na 124 vya Sheria ya Masako ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 (kama ilivyorekebishwa).

## 58. MAELEZO YA UJUMLA

a) Maombi ya kununua vipande katika mazingira yafuatayo, yanaweza kukataliwa na Meneja:

   i. Maombi yamepokelewa pamoja na fedha pungufu ya kima cha chini kinachoruhusiwa kwa ajili ya kununua vipande;
   ii. Fomu ya Maombi haikutiwa saini na mwombaji;
   iii. Mwombaji hana sifa za kuwekeza kwenye Mfuko;
   iv. Hundi iliyopelekwa benki ikiwa ni pamoja na maombi imekataliwa na malipo hayakupokelewa na Meneja.

b) Uamuzi wowote wa Meneja wa Mfuko kuhusu kustahili au kutostahili kwa mwombaji kujiunga na Mfuko, utakuwa ni wa mwisho baada ya kuthibitishwa na Mamlaka. Kurejeshwa kwa fedha ya maombi yaliyokataliwa kutafanyika baada ya taratibu za kiutendaji kutekelezwa kwa gharama ya mwombaji na Meneja hatawajibika kulipa riba au kiasi kingine chochote cha fedha.

c) Wamiliki ambao umiliki wao umetokana na udanganyifu katika maelezo yao, utafutwa na majina yao kuondolewa katika daftari la wenye vipande. Katika hali kama hiyo, Meneja atakuwa na haki ya kununua tena umiliki wa vipande hivyo kwa bei ya mwanzo au katika

thamani halisi ya kipande ya wakati huo kutegemea bei ipi itakuwa ndogo kati ya hizo, baada ya kutoza kiasi ambacho ni sawa na asilimia kumi (10%) ya bei ya kununulia kama adhabu.

d) Africa Pension Fund Limited (APeF), katika nafasi yake kama Meneja wa Mfuko, inahifadhi haki ya kurekebisha, kubadilisha au kusahihisha masharti na vigezo vya Waraka wa Toleo hili mara kwa mara. Mabadiliko yoyote yatakayobadilisha mambo ya msingi ya waraka wa toleo hili yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa ajili ya kupata idhini ya awali, kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazotumika. Baada ya kuidhinishwa, marekebisho yote yatawasilishwa kwa wawekezaji kupitia tovuti ya Africa Pension Fund Limited na kwa tangazo la umma katika magazeti yanayosambazwa kwa wingi. Mabadiliko hayo yataanza kutumika kuanzia tarehe itakayotajwa katika mawasiliano husika.

### 59. ADA NA MAKATO

Hakutakuwa na gharama kwa mauzo ya awali. Gharama zote za awali zitalipwa na Meneja wa Mfuko

### 60. KIFO CHA MWEKEZAJI

a) Endapo mmoja wa wamiliki wa Pamoja (joint) wa vipande atafariki, mwekezaji aliyebaki ndiye atakayekubalika na Mfuko kama mwenye haki ya umiliki au maslahi katika vipande vinavyoonekana katika Taarifa ya Akaunti.
b) Iwapo uteuzi wa mrithi umefanywa, vipande vitamilikiwa na mrithi mara baada ya kifo cha mwekezaji wa vipande. Baada ya kukamilisha taratibu zote zinazohitajika, mrithi atapewa Taarifa ya Akaunti kwa vipande hivyo. Hii haiondoi haki za mtu mwingine yeyote mwenye madai dhidi ya vipande hivyo.
c) Iwapo hakuna mrithi, basi msimamizi wa mirathi ndiye atakayekubalika na Mfuko kama mwenye haki ya umiliki wa vipande. Msimamizi wa mirathi ataandikishwa kama mwekezaji wa vipande na Taarifa ya Akaunti itatolewa kwa jina lake.
d) Endapo hakuna mrithi, mtu yeyote mwenye haki ya kupata vipande kutokana na kifo cha mwekezaji wa vipande peke yake au wote wawili wa umiliki wa pamoja, baada ya kutoa ushahidi wa kutosha, anaweza ama kuandikishwa kama mwekezaji wa vipande hivyo kwa kutoa taarifa kwa Mfuko kwa maandishi au kuhamisha vipande hivyo kwa mtu mwingine.
e) Masharti yote ya vikwazo, mipaka, na masharti mengine ya Mfuko kuhusu uhamisho yatatumika kwenye taarifa au uhamisho huo kana kwamba kifo hakikutokea na uhamisho umefanywa na mwekezaji wa awali wa vipande.
f) Mfuko unaweza kushikilia fedha yoyote inayolipwa kwa vipande ambavyo mtu anastahili hadi pale mtu huyo atakapojisajili kama mwekezaji wa vipande au kuhamisha vipande kwa mujibu wa sheria za Mfuko.

### 61. MANUFAA YATAKAYOTOLEWA WAKATI WA KIFO

Iwapo kifo cha mwekezaji wa vipande kitatokea, mrithi halali atastahili kupata manufaa yafuatayo:

a) Thamani halisi ya vipande vilivyopo kwa wakati huo – Italipwa na Mfuko;
b) Kiasi cha Bima ya Maisha kinachostahili – Italipwa na Mtoa Bima

Iwapo kifo cha bahati mbaya cha mtoto wa mwekezaji wa vipande, mwekezaji wa vipande atastahili kupata manufaa yafuatayo:

Kiasi cha Bima ya Mazishi kulingana na stahili ya thamani ya vipande vyake – Italipwa na Mtoa Bima.

## 62. MANUFAA YATAKAYOTOLEWA – ULEMAVU WA WAKUDUMU

Endapo mwekezaji atapata ulemavu wa wakudumu iwe kutokana na ugonjwa au ajali basi mlezi atastahili kupata manufaa yafuatayo:

a) Thamani halisi ya vipande vilivyopo kwa wakati huo – Italipwa na Mfuko;
b) Kiasi cha Bima ya Ulemavu wa Kudumu kinachostahiki – Italipwa na Mtoa Bima.

## 63. MIKUTANO

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa wawekezaji kila mwaka kama ifuatavyo:

a) Mwekezaji ataruhusiwa kuteua mwakilishi ili kumwakilsha kwenye mkutano.
b) Kura zitategemea uwiano wa idadi ya vipande.
c) Ili maazimio yaweze kufanyika, akidi ya mkutano maalum au wa dharura itakuwa ni asilimiaishirini na tano (25%) ya vipande vilivyotolewa na asilimia kumi (10%) kama ni mkutano wa kawaida wa mwaka.
d) Kama akidi haijatimia na imepita nusu saa baada ya muda uliopangwa kuanza mkutano, mkutano utaahirishwa kwa siku zisizopungua kumi na tano (15). Akidi ya huo mkutano baada ya kuahirishwa itakuwa ni wawekezaji watakaokuwepo au wawakilishi wao.
e) Mkutano mkuu maalum unaweza kuitishwa ili:
    i. Kurekebisha, kubadilisha au kuongeza, kupunguza makubaliano katika waraka wa udhamini.
    ii. Kufunga mfuko.

Mdhamini, Meneja hawataruhusiwa kupiga kura au kuhesabiwa kama akidi katika mkutano ambao wana maslahi.

Maamuzi ya mkutano mkuu wa kawaida yatapitishwa kwa kuangalia wingi wa kura za wawekezaji waliopo na wenye haki ya kupiga kura kwa kuwepo wenyewe au wawakilishi wao. Maamuzi ya mkutano mkuu maalum yatapita endapo yamepitishwa kwa asilimia sabini na tano au zaidi ya kura za umiliki wa Mfuko wa wawekezaji waliopo au wawakilishi wao.

| | |
|---|---|
| Ofisi:<br>Office/Branch ______________________ | **Fomu ya Kufungua Akaunti<br>(Account Opening Form)** |
| Tarehe (Date) ______________________ | |

**Mimi/Sisi tunapenda kufungua akaunti kwa ajili ya uwekezaji na ununuzi wa vipande vya mfuko unaosimamiwa na Africa Pension Fund (APeF) kwa kutoa taarifa zifuatazo:**
**(I/We hereby wish to open an account for the subscription and redemption of fund units managed by Africa Pension Fund (APeF) with the provision of the following information)**

**Akaunti za Pamoja: Miamala yote (mauzo, manunuzi, mahamisho na kufunga akaunti) katika akaunti za pamoja itafanyika baada ya kuthibitishwa kwa kutia saini kwa wamiliki wote.**
**Mnufaika aliyesalia: Mmiliki/ Wamiliki wa akaunti akifariki wamiliki waliobaki watakuwa na haki miliki baki katika akaunti**

**Joint Accounts: Shall be operated Jointly by All Holders, meaning all transactions (including withdrawal, transfer, or closure) require the signature/instruction of all registered joint account holders.**
**Survivorship: Upon the death of any one or more joint holder(s), the entire balance and rights to the account shall vest in the surviving holder(s).**

| Aina ya Akaunti: (Account Type) | Binafsi: ☐ (Individual) | Akaunti ya Pamoja: ☐ (Joint) | Kampuni/Taasisi/Kikundi: ☐ (Company/Institution/Group) | Mtoto: ☐ (Minor) |
|---|---|---|---|---|

**SEHEMU A (SECTION A)**
**TAARIFA YA MWEKEZAJI WA KWANZA (1ST INVESTOR'S INFORMATION)**

| | | |
|---|---|---|
| Jina la Kwanza (First Name) | Jina la Kati (Middle Name) | Jina la Ukoo (Surname) |
| Tarehe ya Kuzaliwa (Date of Birth) | Jinsia: (Gender) — Mwanaume (Male) ☐ Mwanamke (Female) ☐ | Uraia (Nationality) |

| Aina ya Kitambulisho: (Identification Type) | Kitambulisho cha Uraia (NIDA) ☐ | Pasipoti (Passport) ☐ | Leseni ya Udereva (Driver's License) ☐ | Kadi ya Mpiga Kura (Election Card) ☐ |
|---|---|---|---|---|

| | |
|---|---|
| Namba ya Kitambulisho (Identification Number) | Namba Ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN) |
| Namba ya Simu (Mobile No) | Barua Pepe (Email) |
| Sanduku la Posta (Postal Address) | Anuani ya Makazi (Physical Address) |
| Wilaya (District) | Province (Jimbo) |
| Region (Mkoa) | Country (Nchi |

**SEHEMU B (SECTION B)**
**TAARIFA YA MWEKEZAJI WA PILI (2ND INVESTOR'S INFORMATION)**

| | | |
|---|---|---|
| Jina la Kwanza (First Name) | Jina la Kati (Middle Name) | Jina la Ukoo (Surname) |
| Tarehe ya Kuzaliwa (Date of Birth) | Jinsia: (Gender) — Mwanaume (Male) ☐ Mwanamke (Female) ☐ | Uraia (Nationality) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Aina ya Kitambulisho: (Identification Type) | Kitambulisho cha Uraia (NIDA) ☐ | Pasipoti (Passport) ☐ | Leseni ya Udereva (Driver's License) ☐ | Kadi ya Mpiga Kura (Election Card) ☐ |

| | |
|---|---|
| Namba ya Kitambulisho (Identification Number) | Namba Ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN) |
| Namba ya Simu (Mobile No) | Barua Pepe (Email) |
| Sanduku la Posta (Postal Address) | Anuani ya Makazi (Physical Address) |
| Wilaya (District) | Province (Jimbo) |
| Mkoa (Region) | Country (Nchi) |

**SEHEMU C (SECTION C)**
**TAARIFA YA TAASISI/KAMPUNI/KIKUNDI (COMPANY/INSTITUTION/GROUP INFORMATION)**

| | |
|---|---|
| Jina la Kampuni/Taasisi/Kikundi (Name of Company /Institution/Group) | Namba ya Usajili (Registration No) |
| Cheti cha Usajili: (Certificate of Registration) NDIO(YES) ☐ HAPANA (NO) ☐ | Nchi ya Usajili (Country of Registration) |
| Aina ya Biashara (Type of Business) | Namba ya Simu (Phone Number) |
| Barua Pepe (Email Address) | Sanduku la Posta (Postal Address) |
| Anuani ya Makazi (Physical Address) | Wilaya (District) |
| Province (Jimbo) | Mkoa (Region) |
| Country (Nchi) | |

**Tafadhali Ambatanisha Nyaraka Zifuatazo (Please Attach the Following Documents)**

| | | |
|---|---|---|
| Cheti cha BRELA (BRELA Certificate) ☐ | Cheti cha Mlipa Kodi (TIN Certificate) ☐ | Leseni ya Biashara (Business License) ☐ |
| Idhini ya Bodi (Board Resolution Authorizing Account Opening) ☐ | | |

**Wasaini Walioidhinishwa**
**(Authorized Signatories)**

| Jina (Name) | Sahihi (Signature) |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |

**SEHEMU D (SECTION D)**
**TAARIFA ZA KIBENKI ZA MWEKEZAJI (INVESTOR'S BANK DETAILS)**

| | |
|---|---|
| Jina la Benki (Bank Name) | Tawi la Benki (Bank Branch) |
| Jina la Akaunti (Account Name) | Nambari ya Akaunti (Account Number) |

**SEHEMU E (SECTION E)**
**CHANZO CHA KIPATO (SOURCE OF INCOME)**

| | | |
|---|---|---|
| Mshahara: (Salary) ☐ | Biashara: (Business) ☐ | Vyanzo Vinginevyo: (Others) ☐ |

| Tafadhali Fafanua kama Umechagua Vyanzo Vinginevyo (Please Specify if You have Chosen Others) |
|---|

**SEHEMU F (SECTION F)**
**TAARIFA ZA WARITHI (DETAILS OF NOMINEES)**

| S/N | Jina Kamili (Full Name) | Tarehe ya Kuzaliwa (Date of Birth) | Asilimia ya Umiliki (% of Ownership) | Uhusiano (Relationship) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |

**TAARIFA ZA MLEZI WA WARITHI WALIOTAJWA HAPO JUU**
**(GUARDIAN CONTACT INFORMATION FOR NOMINEES LISTED ABOVE)**

| | |
|---|---|
| Jina Kamili (Full Name) | Tarehe ya Kuzaliwa (Date of Birth) |
| Anuani ya Makazi (Physical Address) | Namba ya Simu (Phone Number) |
| Relationship with Nominees (Uhusiano na Warithi) | |

| Aina ya Kitambulisho: (Identification Type) | Kitambulisho cha Uraia (NIDA) | Pasipoti (Passport) | Leseni ya Udereva (Driver's License) | Kadi ya Mpiga Kura (Election Card) |
|---|---|---|---|---|
| | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |

**SEHEMU H (SECTION G)**
**TAARIFA ZA MALIPO (PAYMENT DETAILS)**

| | |
|---|---|
| Kiasi Kilicholipwa (kwa Tarakimu Tzs): (Paid Amount in Figures Tzs) | |
| Kiasi Kilicholipwa (kwa Maneno Tzs): (Paid Amount in Words Tzs) | |

**SEHEMU I (SECTION H)**
**TAMKO LA UTHIBITISHO (DECLARATION)**

Mimi/Sisi tunathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapa ni za kweli, kamili na sahihi kwa kadri ya ufahamu wangu/wetu. Mimi/Sisi tunakubali kuiarifu Africa Pension Fund Limited mara moja endapo kutatokea mabadiliko yoyote ya taarifa hizi.
(I/We confirm that the information provided herein is true, complete and accurate to the best of my/our knowledge. I/We agree to promptly inform Africa Pension Fund Limited of any changes to this information.)

| | |
|---|---|
| Jina la Mwekezaji Mkuu (Primary Applicant's Name) | Sahihi (Signature) |
| Jina la Mwekezaji wa Pili (Secondary Applicant's Name) | Sahihi (Signature) |

We confirm receipt of the application and supporting documents as submitted by the applicant. The accuracy and completeness of the information provided remain the responsibility of the applicant, and the application will be processed in line with APeF's Standard Onboarding Procedures
Tunathibitisha kupokea fomu ya ombi la kufungua akaunti pamoja na nyaraka husika kama zilivyowasilishwa na mwombaji. Usahihi na ukamilifu wa taarifa zilizotolewa unabaki kuwa jukumu la mwombaji, na ombi litashughulikiwa kwa mujibu wa Taratibu za Kawaida za Kufungua Akaunti za APeF.

| | |
|---|---|
| Imefunguliwa Na (Account Opened By) | |
| Imeidhinishwa Na (Authorized By) | |
| KYC Level: 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ | |
| Namba ya Akaunti ya Mwekezaji:<br>(Investor's Account Number) | |

# WASILIANA NASI

SKANI
HAPA KWA
TAARIFA ZAIDI

apef@apef.co.tz apeftanzania

Piga bure **0800 11 1234** www.apef.co.tz

Ghorofa ya pili, Jengo la Tawi la Benki ya Exim-Masaki
Barabara ya 153, Haile Selassie, Dar es salaam